**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO

**DKT. SAADA MKUYA SALUM (MBM)**

# KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Juni, 2023**



**“Tutashirikiana kujenga Uchumi mpya kwa Umoja, Mshikamano na Maridhiano”**

Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

## YALIYOMO


A. UTANGULIZI ........................................................................ 1
B. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI JULAI
2022 – MACHI 2023 ................................................................ 3
a. Mapato ya Serikali Julai-Machi 2022/2023 ................................... 3
b. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) 4
c. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) 4
d. Mapato yasiyokuwa ya Kodi ........................................................ 4
e. Mapato yatokanayo na Mamlaka ya Serikali za Mitaa .................. 4
f. Mapato ya Washirika wa Maendeleo ........................................... 5
g. Matumizi ya Serikali kwa Kipindi cha Julai-Machi 2022/2023 ....... 6
h. Matumizi ya Kazi za Kawaida ...................................................... 7
i. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ................................................ 8
j. Matumizi ya Huduma Mfuko Mkuu wa Serikali .............................. 8
C. MISAMAHA YA KODI ILIYOTOLEWA KWA KIPINDI CHA
JULAI 2022 –MACHI 2023 .......................................................... 8
D. DENI LA TAIFA ......................................................................... 9
E. UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA SERA ZA MAPATO KWA
MWAKA WA FEDHA 2022/2023 .................................................. 9
Hatua zinazohusu Marekebisho ya Sheria .................................. 10
E.1 Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka, 1998 ........... 10
E.2 Sheria ya Ushuru wa Stempu nambari 7 ya mwaka 2017 ............ 11
E.3 Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015 ................................. 12
E.4 Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Barabarani Namba 7 ya
mwaka 2003 ............................................................................ 12
E.5 Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya
mwaka 2016. ........................................................................... 13
E.6 Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi Nambari 7 ya
Mwaka 2009. ........................................................................... 13
E.7 Sheria ya kukuza uwekezaji Zanzibar namba 14 ya mwaka 2018 14
F. Hatua za Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi .................. 14
F.1 Uunganishaji wa Mifumo ya Forodha (TANCIS), Usajili wa
Gari (MVLRS) na Mfumo wa VFMS. ........................................... 14
F.2 Kuanza kukusanya kodi ya mapato kwa Kampuni za kigeni
za usafirishaji (non - resident person) ....................................... 14

G. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 HADI JUNI 2023 .......... 15
a) Matarajio ya Mapato Julai 2022-Juni 2023 .......... 15
b) Matarajio ya Matumizi Julai 2022-Juni 2023 .......... 16
H. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA MWAKA JULAI 2022-MACHI 2023. .......... 16
I. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2023 .......... 46
K. SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2023/2024 .......... 54
L. HALI YA UTEGEMEZI KWA MWAKA 2023/2024 .......... 56
M. MAZINGATIO YA MAENEO MAHSUSI KWA MATAYARISHO YA BAJETI YA MWAKA 2023/2024 .......... 56
N. SHUKRANI .......... 57
O. HITIMISHO .......... 59
A. VIAMBATISHO .......... 60

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, tukiwemo sisi waja wake. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote uzima na uwezo wa kukutana tena leo tukiwa katika hali njema ya afya na amani ambayo inatuwezesha kufanya shughuli zetu tukiwa na utulivu. Yote haya yanawezekana kwa sababu ya neema zake anazoendelea kuturuzuku. Tumuombe Mola wetu atuzidishie amani nchini kwetu ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa faida ya nchi na wananchi wenzetu tunaowawakilisha.

2. **Mheshimiwa Spika,** fursa hii ulionipa inanipa nafasi ya kutimiza matakwa ya Kifungu cha 105 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 kinachomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha, kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaofuata. Kwa dhamira hiyo, naomba kutoa hoja kuwa Baraza lako sasa likae kama Kamati ya kujadili na hatimae kuidhinisha mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

3. **Mheshimiwa Spika,** katika vikao kama hivi ambavyo hukutana na kupitia mipango yetu ya maendeleo na mapendekezo ya Bajeti kwa sekta zote, kipindi hichi kimekuwa cha kipekee ambacho kimeonesha mashirikiano mazuri ya kidugu na utulivu. Wananchi wa Zanzibar kwa ujumla wetu wameudhihirishia ulimwengu kuwa tunaweza kuishi kwa amani, utulivu na mshikamano bila ya kujali tofauti zilizopo miongoni mwetu. Tumuombe Mwenyezi Mungu atuzidishie amani hii na umoja wetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Tukumbuke kuwa mafanikio makubwa tunayoyaona leo yanatokana na kazi kubwa inayofanywa na kiongozi wetu, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambae amekua akifanya kazi usiku na mchana katika kusimamia utekelezaji wa ahadi zake kwa

Wazanzibari. Mafanikio haya tunayojivunia leo ya amani, utulivu na umoja wetu ni ishara ya uongozi wake uliotukuka, na unaopendelea mema nchi yetu. Hatuna budi pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kupata Viongozi waadalifu na imara chini ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakiongozwa na Mwenyekiti mahiri, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akisaidiwa na Makamo wake kwa upande wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambao tunaona wazi jitihada zao katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

5. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku, Mheshimiwa Rais amekuwa akifanya kazi kwa karibu sana na wasaidizi wake wakuu. Hivyo, wakati tukimpongeza Mheshimiwa Rais kwa mafanikio yake, naomba pia uniruhusu kuwapongeza sana wasaidizi wake wakuu Mheshimiwa Othman Masoud Othaman Makamo wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamo wa Pili wa Rais kwa jinsi wanavyomsaidia kiongozi wetu katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuliendesha taifa hili. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awazidishie busara na hekima viongozi wetu ili waendelee kuiongoza nchi yetu kwa amani, utulivu na kujenga misingi ya uchumi ulio imara.

6. **Mheshimiwa Spika,** tukio letu la leo, linakwenda kubakia katika historia ya nchi yetu, hivyo uwepo wangu leo hapa ni safari iliyoanza mbali, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti **Mheshimiwa Abdallah Hussein Kombo** Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani na wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti. Kwa wakati huu pia nawashukuru Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa uchambuzi wa kina wa taarifa zilizomo katika Bajeti ya mwaka 2023/2024 na michango waliyotupatia, ambayo pia imezingatiwa katika matayarisho ya Bajeti ninayoiwasilisha.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia nitumie fursa hii adhimu kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa imani yake aliyoiweka

kwangu na kunipa jukumu hili muhimu kwa nchi yetu na kuendelea kuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi nikiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Natambua kuwa Ofisi hii ndiyo moyo kwa Serikali yetu, hivyo nitaendeleza ahadi yangu kwake ya kujituma kwa nguvu, maarifa na uzoefu wangu wote ili kutimiza malengo ya nchi yetu.

8. **Mheshimiwa Spika,** ikiwa naelekea kuwasilisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali, naomba pia Baraza lako liizingatie hotuba niliyoiwasilisha asubuhi ya leo kuwa ni sehemu ya mazingatio na muendelezo wa hotuba hii. Hivyo, naomba tuuzingatie kuwa Mwenendo wa Hali ya Uchumi ya Zanzibar kwa mwaka 2023 sawia na ule niliouwasilisha katika Hotuba ya Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024.

## B. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI JULAI 2022 – MACHI 2023

9. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, imekadiria kukusanya na kutumia TZS 2,606.58 bilioni. Kati ya fedha hizo TZS 2,572.7 bilioni zimepangwa kukusanywa na kutumika na Serikali Kuu na TZS 33.88 bilioni zimepangwa kukusanywa na kutumika na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### a. Mapato ya Serikali Julai-Machi 2022/2023

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2022 - Machi 2023, Serikali imefanikiwa kukusanya TZS 1,110.65 bilioni sawa na asilimia 43 ya bajeti ya kukusanya kwa mwaka ya TZS 2,606.58 bilioni na asilimia 75 kwa makadirio ya Julai - Machi ya kukusanya TZS 1,482.00 bilioni. **(Kiambatisho Namba 1).**

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilikadiria kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya TZS 1,369.75

bilioni. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya TZS 902.57 bilioni zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 83 ya makadirio ya TZS 1,090.31 bilioni na asilimia 66 kwa Bajeti ya Mwaka.

**b. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2022/2023, Mamlaka ya Mapato Zanzibar imekadiriwa kukusanya TZS 579.51 bilioni. Hadi kufikia Machi 2023, Mamlaka imekusanya TZS 449.26 bilioni sawa na asilimia 78 ya lengo la mwaka na asilimia 97 kwa makadirio ya Julai - Machi 2022/2023 ya TZS 462.49 bilioni.

**c. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar**

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2022 - Machi 2023, TRA kwa upande wa Zanzibar imekusanya TZS 323.01 bilioni sawa na asilimia 71 ya bajeti ya Mwaka ya TZS 454.06 bilioni na asilimia 96 kwa makadirio ya kipindi cha tathmini ya TZS 337.03 bilioni.

**d. Mapato yasiyokuwa ya Kodi**

14. **Mhesimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 - Machi 2023, mapato yasiyokuwa ya kodi yaliyokusanywa yamefikia TZS 116.30 bilioni sawa na asilimia 65 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 179.48 bilioni na asilimia 83 kwa makadirio ya kukusanya TZS 139.35 bilioni kwa kipindi cha tathmini.

**e. Mapato yatokanayo na Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

15. **Mhesimiwa Spika,** Kwa upande Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 makusanyo halisi yamefikia TZS 27.59 bilioni sawa asilimia 91 ya makadirio ya miezi tisa ya TZS 30.16 bilioni na asilimia 81 ya makadirio ya TZS 33.88 bilioni ya bajeti ya mwaka.

### f. Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

16. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ilitarajia kupokea TZS 687.95 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai - Machi 2022/2023 fedha zilizopokelewa ni TZS 180.49 bilioni sawa na asilimia 26 ya makadirio ya mwaka na asilimia 75 kwa kipindi cha tathmini: fedha hizo zimepatikana katika maeneo yafuatayo:

i. TZS 80.14 bilioni Mikopo nafuu iliyoelekezwa katika program na miradi sawa na asilimia 13 ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023;
ii. TSZ 32.69 bilioni ni misaada kwa ajili ya utekelezaji wa program na miradi sawa na asilimia 46 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 70.86 na asilimia 65 kwa kipindi cha tathmini;
iii. TZS 67.43 bilioni zinatokana na Misaada ya Kibajeti (GBS). Makadirio ya mwaka ilikuwa ni kupokea TZS 10.00 bilioni; na
iv. TZS 230 milioni zinatokana na Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (Basket Fund) sawa na asilimia 100 ya makadirio ya mwaka.

**Misaada ya Kibajeti (General Budget Support)**

17. **Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kwa juhudi kubwa kutafuta fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Fedha zinazotoka kwa Washirika wa Maendeleo, hupokelewa kupitia njia tofauti ikiwemo Miradi ya moja kwa moja ya Kisekta (Direct Project Financing), Mifuko ya Pamoja (Basket Funds) pamoja na Misaada ya Kibajeti (General Budget Support - GBS). Kupitia utaratibu wa GBS, Zanzibar kwa kipindi kirefu imekua ikipokea kiwango kidogo cha asilimia 4.5 ambacho hakikuweza kuakisi mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Kupitia Awamu mbali mbali, SMZ imekua ikifanya juhudi mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kuangalia uwezekano wa kuongeza kiwango hicho ili kiendane na hali halisi ya mahitaji yaliyopo.

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua , umuhimu wa suala hili kisiasa, Viongozi wetu Wakuu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt.Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, waliagiza kwa pande zote mbili kukaa pamoja na kuangalia misingi na vigezo vya kitaalamu vitakavyokuwa bora katika ugawaji wa rasilimali hizo kwa pande zetu mbili. Baada ya Kamati za Kitaalamu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukaa kwa pamoja na kulifanyia kazi suala hilo, mapendekezo yaliyozingatia vigezo vya kiuchumi, kiutawala pamoja na uwezo wa kukopa, yamewasilishwa na kupokelewa na Serikali ambapo kuanzia sasa, mgao wa GBS kwa Zanzibar umeongezeka na kufikia asilimia 9 badala ya asilimia 4.5 iliyokuwepo awali.

19. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, nachukua fursa hii, kuipongeza kwa dhati, Kamati ya Wataalamu waliolisimamia jambo hili hadi kufikia makubaliano. Aidha, tunawashuruku na kuwapongeza kwa dhati, Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa umahiri na umakini wao pamoja na uthubutu wa kusimamia uchumi, ustawi wa jamii na maendeleo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nikweli usiofichika kuwa Zanzibar inafaidika ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania……….!! **”Kazi Inaendelea”**…... na hakuna atakaebisha kuwa **Yajayoooo…! “Ni Neema Tupu”….!!**

### g. Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Julai-Machi 2022/2023

20. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai - Machi Mwaka wa Fedha 2022/2023, matumizi halisi yalifikia TZS 1,030.53 bilioni, sawa na asilimia 40 ya makadirio ya Bajeti ya Mwaka ya TZS 2,606.58 billioni na asilimia 77 ya kipindi cha tathmini. Matumizi haya yamejumuisha matumizi ya TZS 731.17 bilioni zilizotumika kwa kazi za kawaida na TZS 273.33 bilioni zimetumika kwa Matumizi ya kazi za Maendeleo na Matumizi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni TZS 26.03 bilioni.

### h. Matumizi ya Kazi za Kawaida

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida TZS 731.17 bilioni zimetumika sawa na asilimia 60 ya bajeti ya 1,220.51 bilioni iliyopangwa kwa Mwaka na asilimia 79 kwa makadirio ya kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimetumika kwa ufafanuzi ufuatao:

    i. Malipo ya Mishahara ya waajiriwa wa Serikali ni TZS 392.14 bilioni sawa na asilimia 70 kwa Bajeti ya Mwaka ya TZS 557.95 bilioni na asilimia 99 kwa makadirio ya kipindi cha tathmini;
    ii. Malipo ya mishahara kwa Taasisi zinazopokea ruzuku ni TZS 73.3 bilioni sawa na asilimia 104 kwa Bajeti ya Mwaka na asilimia 96 ya makadirio ya malipo kwa kipindi cha tathmini. Sababu ya ongezeko hilo ni mabadiliko ya mishahara mipya kwa watendaji wa Taasisi za Serikali.
    iii. Malipo ya Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali ni TZS 127.90 bilioni sawa na asilimia 61 ya Makadirio ya Mwaka ya kutumia TZS 210.30 bilioni na asilimia 90 ya makadirio ya kutumia TZS 141.82 bilioni kwa kipindi cha tathmini; na
    iv. Matumizi mengineyo ya Serikali ni TZS 137.84 bilioni sawa na asilimia 36 ya makadirio ya mwaka ya TZS 381.53 bilioni.

### Malipo ya Mishahara kwa Madiwani

22. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeanza kulipa mishahara kwa Madiwani wote wa Zanzibar kutoka fungu kuu la mshahara ili kuweka mazingira bora ya utendaji kwa wananchi wanaowahudumia. Hatua hii imeamsha ari ya utendaji kwa Waheshimiwa Madiwani kufuatilia kwa karibu huduma kwa wananchi wa Zanzibar. Hadi kufikia Machi TZS 1.02 bilioni zimetumika kwa kuwalipa Madiwani 210 wakiwemo Meya 5.

### i. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

23. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 matumizi ya Miradi ya Maendeleo yalifikia TZS 273.33 bilioni sawa na asilimia 20 ya bajeti ya mwaka na asilimia 65 kwa kipindi cha tathmini. Kati ya matumizi hayo, TZS 172.27 bilioni zimetokana na fedha za ndani sawa na asilimia 25 ya bajeti ya mwaka na asilimia 80 ya kipindi cha tathmini. TZS 31.84 bilioni ni Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 51 ya bajeti ya mwaka na fedha za mikopo zilizotumika ni TZS 69.22 bilioni sawa na asilimia 11 ya bajeti ya mwaka.

### j. Matumizi ya Huduma Mfuko Mkuu wa Serikali

24. **Mheshimiwa Spika,** huduma ya Mfuko Mkuu wa Serikali umepangiwa kutumia jumla ya TZS 210.30 bilioni kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2022/2023 jumla ya TZS 127.90 bilioni zimetumika sawa na asilimia 90 ya kutumia TZS 141.82 bilioni kwa kipindi cha Tathmini na asilimia 61 kwa bajeti ya Mwaka. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Malipo ya mafao ya Kiinua Mgongo ni TZS 18.70 bilioni kwa malipo ya Wastaafu 740;
ii. Malipo ya Pencheni kwa wastaafu wa SMZ ni TZS 19.55 bilioni ikiwa ni malipo kwa wastani wa Wastaafu 13,439;
iii. Malipo ya Mikopo ya ndani TZS 30.14 bilioni ikiwemo marejesho ya Mkopo uliochukuliwa kutoka ZSSF ni TZS 7.51 bilioni; na
iv. Matumizi ya mengineyo ya Serikali TZS 59.51 bilioni.

## C. MISAMAHA YA KODI ILIYOTOLEWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023

25. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miezi tisa maombi 287 ya misamaha ya kodi kutoka Taasisi za Umma, Taasisi zisizo za Kiserikali na taasisi binafsi yamewasilishwa ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 28.6 ikilinganishwa na maombi yaliyowasilishwa kipindi

cha tathmini kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ambapo jumla ya maombi 223 yaliwasilishwa. Kati ya maombi hayo, jumla ya maombi 174 yenye thamani ya TZS 65.7 bilioni yamekubaliwa kutokana na kukidhi masharti ya Sheria na Kanuni za Misamaha. Misamaha hii inaonesha ongezeko la TZS 40.3 bilioni ikilinganishwa na misamaha ya TZS 25.4 bilioni iliyotolewa katika kipindi hichi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ongezeko la maombi ya misamaha hiyo limetokana na kuongezeka kwa Miradi ya Wawekezaji pamoja na Miradi ya Washirika wa Maendeleo pamoja na Taasisi Zisizo za Kiserikali ambapo inailazimu Serikali kusamehe mapato ili kupunguza gharama za miradi hiyo.

## D. DENI LA TAIFA

**26. Mheshimiwa Spika,** Deni linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi kufikia Machi 2023 limefikia TZS 330.40 bilioni ambapo kati ya deni hilo, deni la ndani ni TZS 317.17 billion sawa na asilimia 96 ya deni lote na deni la nje ni TZS 13.20 bilioni sawa na asilimia 4 ya deni lote.

**27. Mheshimiwa Spika,** kati ya deni la TZS 317.17 bilioni, Hati Fungani za muda mrefu ambazo zilizochukuliwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania ambazo zimechukuwa uzito mkubwa kufikia TZS 279.50 bilioni sawa na asilimia 87.7 ya deni la ndani na mikopo kutoka Mfuko wa Hifadhi wa Jamii (ZSSF) umefikia TZS 37.65 bilioni sawa na asilimia 12.3 ya deni la ndani. Deni la nje linalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Zanzibar limefikia TZS 2,381.73 bilioni sawa na Dola za Kimarekani 1,030.41 milioni.

## E. UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA SERA ZA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**28. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23, Baraza la Wawakilishi liliridhia mapendekezo ya Serikali ya kuchukua hatua kadhaa ili kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa Mapato

ya Serikali. Hatua hizo zilihusisha marekebisho ya Sheria pamoja na Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi. Muhtasari wa utekelezaji wa hatua hizo ni kama ifuatavyo; -

**Hatua zinazohusu Marekebisho ya Sheria**

**E.1 Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka, 1998**

**i. Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Mashine za Kieletroniki za Kutolea Risiti na Karatasi za Kuchapishia Risiti**

29. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye Mashine za Kielektroniki na Karatasi za Kutolea Risiti wakati wa uingizaji na usambazaji (uuzaji). Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya Mashine za Kielektroniki za Kutolea Risiti (POS) 2,330 zimenunuliwa na wafanyabiashara 2,072 wamesajiliwa kutumia mashine hizo.

**ii. Kuimarisha Huduma za Utoaji wa Mikopo kwa Benki za Kiislamu (Islamic Bank)**

30. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia mapendekezo ya Serikali ya kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Huduma za Benki za Kiislamu wakati inapowasilisha bidhaa kwa mteja ili kuhakikisha kwamba Wazanzibari wote wanapata huduma za mikopo kwa unafuu katika taasisi za fedha ikijumuisha wale ambao hawakubaliani na utaratibu wa riba. Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2022.

**iii. Utozaji wa Kodi kwenye Huduma zitolewazo Mitandaoni**

31. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Zanzibar imefanikiwa kutunga Rasimu ya Kanuni za Kodi kwenye Huduma zitolewazo Mitandaoni kwa kuweka utaratibu mzuri wa Usajili na Ulipaji wa

Kodi zitokanazo na huduma zinazotolewa mitandaoni. Hata hivyo, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zinaendelea na mchakato wa kuweka namna bora ya utozaji wa Kodi katika sekta hii.

**iv. Kuingizwa katika Wigo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) watoa Huduma za Kitaalamu (Professional Services Providers)**

**32. Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuwaingiza katika wigo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) watoa Huduma za Kitaalamu. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla wa walipakodi 143 wamesajiliwa katika wigo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

**v. Kuimarisha uchumi wa ndani kwa kushajiisha Wawekezaji kununua bidhaa ndani ya nchi**

**33. Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa asilimia 100 kwa Mwekezaji asiyekuwa wa Kimkakati (Non-Strategic Investor) wakati wa ununuzi wa bidhaa za ujenzi nchini, sambamba na kupunguza unafuu wa VAT kutoka asilimia 80 hadi asilimia 75 wakati wa uingizaji wa bidhaa hizo nchini ili kushajihisha Wawekezaji kununua bidhaa ndani ya Nchi. Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2022.

**E.2 Sheria ya Ushuru wa Stempu nambari 7 ya mwaka 2017**

**i. Kuweka usawa wa malipo ya Ushuru wa Stempu kwa wafanyabiashara Wadogo Wadogo**

**34. Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho ili kuleta usawa katika ulipaji wa Ushuru wa Stempu kwa Wafanyabiashara wadogo wadogo kwa mujibu wa mauzo ghafi ya mwaka. Hatua hii imehamasisha wafanyabiashara wadogo wadogo

kujisajili kwa hiari, ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2023, jumla ya wafanyabiashara 1,485 wamesajiliwa katika wigo wa Ushuru wa Stempu.

**ii. Kupunguza viwango vya Ushuru wa Stempu katika Gari za Biashara**

35. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kupunguza viwango vya kutozea Ushuru wa Stempu kwa gari za biashara kwa asilimia 25. Aidha, utekelezaji wa hatua hii, umeongeza uwajibikaji, ulipaji kodi wa hiari, pamoja na kuleta ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**E.3 Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015**

**i. Kutoza Kodi ya Miundombinu katika Vileo**

36. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuanza kutoza kodi ya Miundombinu kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye Vinywaji Vikali, Sigara na Tumbaku wakati wa uingizaji nchini (importation & transfers). Aidha, utekelezaji wa hatua umeanza Septemba, 2022 na jumla ya TZS 2.8 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 80 ya makadirio.

**E.4 Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Barabarani Namba 7 ya mwaka 2003**

37. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia mapendekezo ya Serikali ya kufanya marekebisho ya viwango vya usajili wa vyombo vya moto kama ifuatavyo; -

i. Kupunguza ada ya usajili wa nambari binafsi kutoka TZS 15 milioni kwa miaka mitano hadi TZS 5 milioni kwa miaka mitatu ili kuhamasisha wananchi kuitumia fursa hii. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 gari 5 zimesajiliwa katika usajili wa nambari binafsi ambapo jumla ya TZS 25 milioni zimekusanywa.

ii. Kupandisha ada za usajili wa vyombo vya moto kwa asilimia ishirini (20%) ili kwenda sambamba na mabadiliko ya hali ya uchumi wa Zanzibar kutokana na viwango hivyo kupitwa na wakati kama ifuatavyo; -

   a. Kwa upande wa vyombo vya maringi manne, jumla ya gari 3,295 zimesajiliwa na TZS 428.35 milioni zimekusanywa hadi kufikia Machi, 2023 sawa na ongezeko la TZS 71.10 milioni ikilinganishwa na bei ya zamani.
   b. kwa upande wa vyombo vya maringi mawili jumla ya vyombo 6,407 vimesajiliwa na TZS 480 milioni zimekusanywa sawa na ongezeko la TZS 83.34 milioni ikilinganishwa na bei ya zamani; na
   c. kwa upande wa vyombo vyenye uwezo wa "engine capacity" zaidi ya 50, jumla ya vyombo 644 vimesajiliwa, ambapo TZS 43.24 milioni zimekusanywa ikiwa ni sawa na ongezeko la TZS 7.06 milioni ikilinganishwa na bei ya zamani.

**E.5 Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.**

**i. Kutayarisha Kanuni za miongozo ya Utoaji wa Misamaha ya Kodi**

**38. Mheshimiwa Spika,** Rasimu ya Kanuni ya Miongozo ya Utoaji Misamaha imekamilika na tayari imeshapitishwa na Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango. Rasimu hiyo itawasilishwa katika ngazi mbalimbali Serikalini ili kupata ridhaa ili kuwa na muongozo mmoja wa kutoa misamaha ya kodi.

**E.6 Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi Nambari 7 ya Mwaka 2009.**

**i. Kutayarisha Kanuni za miongozo ya Uwekaji wa Dhamana katika Uendeshaji wa Biashara.**

39. **Mheshimiwa Spika,** masharti ya uwekaji dhamana katika uendeshaji wa biashara yamejumuishwa katika Kanuni ya Jumla ya Sheria ya Usimamizi na Utawala wa Kodi (TAPA) ambayo ipo katika hatua ya kujadiliwa na ngazi ya Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango.

### E.7 Sheria ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar Namba 14 ya mwaka 2018

#### i. Kushajiisha Uzalishaji wa Ndani kwa Wawekezaji wa Kimkakati kwa Kutoa Unafuu wa Malighafi wakati wa Uingizaji

40. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika ilifanyiwa marekebisho kwa kutoa unafuu kwa Wawekezaji wa Kimkakati (Strategic Investors) kuingiza nchini malighafi (raw materials) na pembejeo za viwandani (industrial inputs). Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2022.

## F. Hatua za Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi

### F.1 Uunganishaji wa Mifumo ya Forodha (TANCIS), Usajili wa Gari (MVLRS) na Mfumo wa VFMS.

41. **Mheshimiwa Spika,** mfumo wa TANCIS tayari umeunganishwa na mfumo wa usajili wa magari (Motor Vehicles Licensing and Registration System - MVLRS) na pia unaimarishwa zaidi ili kudhibiti usajili wa gari zinazoingia nchini, na kupata takwimu sahihi za Ankara za Kodi (input tax) kwa waingizaji (importer) pamoja na kufuatilia mwenendo wa walipakodi.

### F.2 Kuanza kukusanya kodi ya mapato kwa Kampuni za Kigeni za Usafirishaji (non - resident person)

42. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2022. Hadi kufikia Machi, 2023 TZS 37.00 milioni zimekusanywa kutokana na kampuni za kigeni za usafirishaji wa abiria na mizigo.

## G. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 HADI JUNI 2023

### a) Matarajio ya Mapato Julai 2022 - Juni 2023

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo, Serikali inatarajia kukusanya 1,719.61 bilioni sawa na asilimia 66 ya Bajeti ya Mwaka ya TZS 2,606.58 bilioni. Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 1,370.35 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023. Taarifa hizi zisomeke kwa pamoja na Kiambatanisho nam.2.

44. **Mheshimiwa Spika,** mapato ya Kodi yanatarajiwa kufikia TZS 1,044.4 bilioni, sawa na asilimia 99 ya bajeti ya TZS 1,054.56 bilioni, kwa mchanganuo ufuatao:
    i. Mamlaka ya Mapato Tanzania - Zanzibar (TRA) inatarajiwa kukusanya TZS 426.60 bilioni ikiwa asilimia 94 ya mapato hayo;
    ii. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inatarajiwa kukusanya TZS 596.79 bilioni ikiwa asilimia 103; na
    iii. Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT inatarajiwa kufikia TZS 21 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

45. **Mheshimiwa Spika,** mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 190.25 bilioni ikiwa ni asilimia 106 kwa mchanganuo ufuatao:-
    i. Mapato ya Mawizara yanategemewa kufikia TZS 163.25 bilioni sawa na asilimia 110.7 ya makadirio ya mwaka ya TZS 147.48 bilioni;
    ii. Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia TZS 15.00 bilioni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mwaka ya TZS 20.00 bilioni; na
    iii. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia TZS 12.00 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya mwaka ya TZS 12.00 bilioni;

46. **Mheshimiwa Spika,** mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yanatarajiwa kufikia Jumla ya TZS 288.67 bilioni sawa na asilimia

42 ya makadirio ya TZS 687.95 bilioni, ambapo misaada inatarajiwa kufikia TZS 43.59 bilioni, mkopo TZS 106.85 bilioni, TZS 0.23 bilioni zinatokana na Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo (Basket Fund) na Misaada ya Kibajeti (GBS) inatarajiwa kufikia TZS 138.00 bilioni. Matarajio ya mkopo utakaochukuliwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo TZS 27.59 bilioni.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa matarajio ni kukusanya TZS 33 bilioni sawa na asilimia 97 ya makadirio.

### b) Matarajio ya Matumizi Julai 2022-Juni 2023

48. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Serikali hadi kufikia Juni 2023 yanatarajiwa kufikia Jumla ya TZS 1,719.61 billioni sawa na asilimia 66 ya bajeti ya mwaka ya TZS 2,606.58 bilioni.
    i. Kati ya fedha hizo TZS 1,003.82 bilioni zitatumika kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 82 ya makadirio; na
    ii. Kwa upande wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo hadi kufikia Juni 2023 inatarajiwa kutumia jumla ya TZS 682.79 bilioni sawa na asilimia 47 ya makadirio ya awali. Kati ya matumizi hayo, TZS 490.34 bilioni ni kutokana na fedha za ndani, TZS 164.86 bilioni ni Mikopo na Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.
    iii kwa upande wa matumizi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa matarajio ni kutumia TZS 33 bilioni sawa na asilimia 97 ya makadirio.

## H. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA MWAKA JULAI 2022 - MACHI 2023.

### a) Sensa ya Watu na Makaazi

49. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekamilisha zoezi la kuhesabu watu katika Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka

2022 lilofanyika Mwezi Agosti 2022 ambayo pia ilijumuisha Sensa ya Majengo na Anwani za Makaazi. Kwasasa Ofisi za Takwimu (Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar) zinaendelea na uchakataji wa taarifa za Sensa na kuandika ripoti mbalimbali kulingana na ratiba ya matoleo ya machapisho ya Sensa. Hadi tarehe 24 Februari, 2023 jumla ya taarifa kumi na moja (11) zimekamilika ambazo zimejikita katika mgawanyo wa idadi ya watu katika maeneo ya kiutawala, mgawanyo wa idadi ya watu kwa umri na jinsi na kuanza kusambazwa kwa wadau mbali mbali wakiwemo viongozi wetu wa kitaifa, waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

50. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya Sensa yanaonesha idadi ya watu nchini Tanzania imeongezeka kutoka Milioni 44.9 Mwaka 2012 hadi Milioni 61.7 Mwaka 2022. Sawa na wastani wa ongezeko la idadi ya watu la asilimia 3.2 kwa upande wa Tanzania na asilimia 3.7 kwa upande wa Zanzibar kwa mwaka. Mkoa wa Mjini Magharibi una asilimia 47.3 ya watu wote waliohesabiwa Zanzibar ikiwa imeongezeka kutoka asilimia 45.5 ikilinganishwa na Sensa ya Mwaka 2012. Ongezeko la asilimia ya idadi ya watu linaonekana pia mkoa wa Kusini Unguja ambapo kulingana na Sensa asilimia hiyo imeongezeka kutoka 8.9 hadi 10.4. Asilimia ya idadi ya watu kwa mikoa ya Kaskazini Pemba, Kusini Pemba na Kaskazini Unguja imeonekana kupungua kutoka Mwaka 2012 hadi Mwaka 2022 kwa viwango tofauti . Mkoa wenye idadi ndogo ya watu nchini ni Kusini Unguja wenye watu laki mbili. Kwa Tanzania Bara, mkoa wenye idadi ndogo ya watu ni Njombe wenye watu laki tisa. Baadhi ya matokeo muhimu yaliyobainika katika Sensa hii ni:

i. Idadi ya wanawake ni wengi kuliko wanaume, ukionyesha uwiano wa kijinsi wa wanaume 95 kwa kila wanawake 100 katika mikoa yote isipokuwa Mkoa wa Kusini Unguja na Mkoa wa Manyara.
ii. Idadi ya watoto walio chini ya umri wa miaka 18 inaendelea kupungua kwa upande wa Zanzibar kutoka asilimia 49 mwaka 2012 hadi asilimia 47.2 mwaka 2022.
iii. Asilimia ya vijana imeendelea kukua kutoka asilimia 20.3 mwaka

2012 hadi 20.4 mwaka 2022. Hawa ni wale wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 kwa mujibu wa tafsiri ya vijana ya Shirika la Kazi Duniani (ILO). Mkoa wenye asilimia kubwa ya vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24 ni Mjini Magharibi (asilimia 21.2).

iv. Kwa ujumla asilimia 1.8 ya watu waliohesabiwa Zanzibari ni wazee wenye umri wa miaka 70. Asilimia 2.3 ya kiwango hicho ni kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja na Mkoa wenye asilimia ndogo ya wazee ni Mkoa wa Mjini Magharibi ambao ni asilimia 1.5 ikilinganishwa na Mikoa mingine ya Zanzibar.

v. Ifikapo mwaka 2025, idadi ya watu Zanzibar inakadiriwa kufikia millioni 2.080; mwaka 2030 tutafikia watu milioni 2.441 na mwaka 2050, Zanzibar inatarajia kufikia watu milioni 4.630. kwa taarifa hii, mipango na mikakati yetu ya kiuchumi, kijamii na kimaendelo inaendelea kuzingatia ongezeko hili la watu.

51. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanza kutumia matokeo haya ya Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2022, katika mipango yake mbali ikiwemo ya elimu na afya na ulipaji wa kodi Serikalini.

### b) Maendeleo ya Sekta ya Utalii

52. **Mheshimiwa Spika,** Serikali bado inaendelea kuimarisha na kuifanya Zanzibar kuwa ni kituo bora cha utalii, ikiwemo juhudi zinazoendelea katika Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na Maeneo ya Kihistoria. Dhamira kuu ni Kuziunganisha na kuziendeleza Sekta za Utalii na Mambo ya Kale kwa lengo la kuyatangaza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini pamoja na, kuuendeleza Mji Mkongwe ambao ni urithi wa kimataifa.

53. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutumia fursa mbali mbali ili kuitangaza Zanzibar na kuwavutia watu kutoka mataifa tofauti kuja kutembelea nchi yetu. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utalii wamefanikiwa kuandaa maonesho ya kwanza ya Utalii na Uwekezaji “Zanzibar Tourism Investment and Travel Exhibition”(ZTITE) yaliyofunguliwa na Mheshimiwa Rais wa

Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika jengo la Beit al Aman, Mnazi Mmoja. Maonesho hayo yaliwakutanisha wanunuzi na wauzaji wa huduma za utalii wa kitaifa na kimataifa. Kufanyika kwa maonesho hayo kunafungua milango kwa Zanzibar katika suala la uwekezaji kwenye sekta ya utalii na kutangazwa zaidi katika masoko ya utalii ndani na nje ya nchi.

54. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imeshinda tuzo ya Bodi bora ya Utalii Afrika 2022 (Best African Tourism Board 2022) iliyotolewa huko Lagos - Nigeria na Pyne Awards 2022 na kupokelewa na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Nd. Rahim Mohamed Bhaloo. Sambamba na hilo, Serikali imeweza kushiriki katika maonesho ya utalii ya Kimataifa kama vile ITB (Internationale Tourismus Börse) – Berlin na Maonesho ya Wazi (Road Show) katika nchi za Ujerumani (Cologne), Uholanzi (Amsterdam), Ubelgiji (Brussels) na Ufaransa (Paris).

55. **Mheshimiwa Spika,** Mikakati hii imetowa matokeo chanya na imepelekea kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini mwaka 2022 na kufikia 548,503 kwa kutoka watalii 394,185 mwaka 2021. Matarajio kwa mwaka 2023 Zanzibar tutapokea watalii 713,053 kutoka nchi za Italia, Ujerumani, Ubelgiji, Uingereza na Spain. Aidha, Serikali inaandaa Makubaliano (MoU) na Jamhuri ya Watu wa China. Kutokana na Amani na Utulivu tulionao katika nchi yetu, idadi ya siku za ukaazi kwa watalii wanaotembelea Zanzibar imeongezeka na sasa mtalii anaweza kutumia wastani wa siku 8 kukaa na kutembelea maeneo tofauti ya Zanzibar.

56. **Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni, Zanzibar imepokea meli nne kubwa za kitalii ambazo ni Zaandam, MS Coral, Geographer na Le Jacques Cartier. Meli hizo ziliwasili nchini na kushusha watalii 1,588 ambao wamepata fursa ya kuvitembelea vivutio mbali mbali vya kitalii ikiwemo mashamba ya viungo, Msitu wa Jozani na maeneo ya Mji Mkongwe.

### c) Uchumi wa Buluu

57. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya nane inayoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, inaendeleza kazi ya kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kiuchumi kupitia sekta ya Uchumi wa Buluu. Uvuvi ikiwa ni sekta ndogo ya Uchumi wa Bluu na inaendelea kuwa ni miongoni mwa shughuli kuu za kiuchumi katika nchi yetu.

58. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka Fedha 2022/2023, Serikali imekamilisha uandaaji wa Sera na Mpango Mkakati wa Uchumi wa Buluu Zanzibar pamoja na Sera na Mpango Mkakati wa Uvuvi Zanzibar. Sera hizo tayari zimeidhinishwa na Baraza la Mapinduzi na zimeanza kutumika Rasmi. Rasimu ya Sheria ya Uvuvi, Sheria ya Uhifadhi na Sheria ya Utafiti wa bahari zimekamilika na zipo ndani ya mchakato wa kuidhinishwa Serikalini. Mpango Mkakati wa mwongozo wa Shirika la Kilimo la Kimataifa (FAO) wa Usimamizi Bora wa Shughuli za Uvuvi mdogo mdogo umekamilishwa na pamoja na miongozo ya usimamizi wa hifadhi za bahari umo ndani ya mchakato wa kuanza kutekelezwa. Mpango Mkuu wa Uvuvi (Fisheries Master Plan) unaendelea kutekelezwa kwa lengo la kuleta ufanisi na kuvutia Sekta binafsi za Uchumi wa Buluu na uwekezaji katika Uvuvi wa Bahari Kuu. Kazi ya Ujenzi wa Diko na Soko la Samaki Malindi umekamilika kwa asilimia 100. Serikali itashirikiana na Sekta binafsi kuhakikisha Soko hilo linaendeshwa kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Mtambo wa kutengeneza Chakula cha Samaki tayari umenunuliwa na Serikali kutoka nchini China, Serikali kwa sasa imo katika maandalizi ya kuifunga mitambo hiyo. Mitambo ya Baridi na mitambo ya kuzalisha barafu yenye uwezo wa kuzalisha tani 200 imefungwa katika soko la Samaki Malindi ili kuwasaidia wajasiriamali wa wavuvi kuweza kuhifadhia bidhaa za baharini. Aidha Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Samaki Mkokotoni Fungu Refu.

**59. Mheshimiwa Spika,** sekta ya Mafuta na Gesi Asilia ni sekta nyengine muhimu katika Uchumi wa Bluu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetumia TZS 947.00 milioni kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi walioathirika na utafiti wa awali wa Mafuta na Gesi Asilia ambao walikuwa wanadai. Fedha hizo ni asilimia 87 ya madai. Serikali inawaomba wale ambao bado hawajalipwa waendelee kuwa wastahamilivu wakati tukiendelea kukamilisha taratibu za malipo yao. Serikali imeshakamilisha awamu ya kwanza ya utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya mtetemo (2D) na sasa ipo katika mchakato wa kuendelea na utafutaji Mafuta na Gesi asili kwa njia ya kina (3D) katika maeneo ya bahari na nchi kavu Unguja na Pemba.

### d) Sekta ya Kilimo

**60. Mheshimiwa Spika,** sekta ya Kilimo inajumuisha sekta ndogo za mazao, mifugo na maliasili za misitu. Sekta hii bado inaendelea kuwa ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa Zanzibar na inachangia moja kwa moja kwenye kipato na uwezo wa wananchi katika kujikimu kimaisha. Sekta ya Kilimo imeajiri takriban asilimia 40 ya wananchi wa Zanzibar wenye uwezo wa kufanya kazi na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hii katika kujikimu kimaisha. Kwa mwaka 2022 Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 22.9 ya Pato la Taifa. Serikali itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji kwa kutumia mbinu bora na teknolojia za kisasa, upatikanaji wa masoko na hatimae kukuza pato la Taifa sambamba na uhifadhi wa maliasili zetu.

**61. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Sensa ya Kilimo iliyofanyika 2019/2020 zimeonesha jumla ya Kaya 180,220 za Zanzibar zinajishughulisha na kilimo ambapo Kaya 162,239 sawa na asilimia 90 ya Kaya hizo zipo katika maeneo ya Vijijini na Kaya 17,981 ikiwa ni asilimia 10 zipo maeneo ya Mjini. Pamoja na kuwepo idadi kubwa ya wanaume wanaojishughulisha na kilimo kama ni shughuli kuu ya kiuchumi katika kujipatia na kujiongeza kipato. Takwimu hizo zimeonesha asilimia 45 ya

wananchi wanaojishughulisha ni wanawake. Hivyo, imani ya Serikali ni kuongeza uwekezaji katika sekta ya kilimo kutawezesha vile vile kuimarika hali za wananchi wetu walio wengi wakiwemo wanawake waliomo katika sekta hii ya kilimo ambao ni tegemeo kubwa katika jamii.

62. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika bonde la Cheju, Kinyasini na Mlemele kwa asilimia 100 ambapo wakulima 4,475 [Cheju (2,500), Kinyasini (1,600) na Mlemele (375)] wamepatiwa konde zao kwa kuendeleza kilimo cha mpunga. Jumla ya tani 88 za mbegu ya mpunga (Unguja tani 50 na Pemba tani 38) zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima, kwa bei ya ruzuku ya asilimia 50. Jumla ya tani 50 za mbolea (ya kupandia tani 30 na kukuzia tani 20) zimenunuliwa kutoka Kampuni ya 'Minjingu Mines and Fertilizers' na SMZ inaendelea na taratibu za kusambazwa kwa wakulima Unguja na Pemba kwa kuchangia gharama za usimamizi.

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mifugo; Serikali imekamilisha tafiti na tathmini ya kuku ambapo imepelekea kupatikana kwa aina tano (5) safi za kuku wa asili (Kuchere, Kawaida, Kibete, Kibutu na Kishingo), sambamba na kupima uzito wa kuku, mayai na kiwango cha chakula wanachotumia. Kwa upande mwengine, Serikali imeshajipanga kuanzisha mkakati wa Kitaifa wa Uhifadhi wa Chakula ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula pindipo ikitokea machafuko yanayoathiri uzalishaji duniani. Hivyo, kwa mwaka 2023/2024, Serikali imetenga jumla TZS 22.50 bilioni kwa ajili ya kutekeleza mkakati mahsusi wa uhifadhi wa chakula (National Food Reserve Strategy) ambayo pamoja na mambo mengine itaangazia namna bora ya kufanya mabadiliko katika sekta ya kilimo ambacho kitaleta tija zaidi katika uzalishaji hapa Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imetenga jumla ya TZS 98.72 bilioni kwa uimarishaji wa Sekta ya Kilimo.

### e) Maendeleo ya Sekta ya Fedha

- **Sekta Ndogo ya Benki**

64. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ndogo ya benki ni moja kati ya sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Sekta hii inajumuisha Benki Kuu ya Tanzania, kama msimamizi mkuu wa shughuli za kifedha katika nchi; benki za biashara; mawakala wa huduma za kibenki; na mitandao ya simu. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, sekta hii imeweza kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi na hivyo kuchangia katika ukuaji wa asilimia 5.4 ya Pato la Taifa.

- **Usimamizi na Udhibiti wa Mifumo ya Malipo Nchini**

65. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2023, mifumo inayotumika katika malipo nchini ikiwemo: *"Digital payment platforms"* na *"Electronic Financial Transfers"* imeendelea kuwa salama na kufanya kazi kwa ufanisi na kurahisha malipo ya Serikali yanayofanyika kwa njia za Mitandao. Utumiaji wa huduma za kifedha kupitia njia ya simu umeendelea kuwa nguzo kubwa ya ushirikishwaji umma katika maswala ya kifedha (Financial Inclusion). Hadi kufikia Machi 2023, idadi ya watu waliokuwa wanatumia simu kupata huduma za kifedha ilifikia asilimia 82.7, ilikinganishwa na asilimia 80.4 iliyofikiwa mwaka 2021/22.

- **Huduma za Kibenki**

66. **Mheshimiwa Spika,** huduma za kibenki hapa Zanzibar zinaendelea kuimarika zikichangiwa zaidi na ukuwaji wa teknolojia, utumiaji wa njia mbadala wa kufikisha huduma kwa wateja ikiwa ni pamoja na mawakala wa benki (Agent Banking). Hadi kufikia mwishoni mwa Machi 2023, idadi ya benki zilizokuwa zikitoa huduma Zanzibar zimefikia 14, huku idadi ya matawi ya benki yakiwa 36, (Pemba ilikuwa na matawi 9 na Unguja ikiwa na matawi 27). Vituo vinavyotowa huduma za utowaji fedha kwa njia ya ATM ni 94 huku idadi ya mawakala wa benki imefikia 1,559 ikijumuisha mawakala

291 waliokuwa Pemba na mawakala 1,268 waliopo Unguja. Maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yaliyosajiliwa (Bureau de Change) yamefikia manne (4) ikiwemo Fast Forex, Posta, Kadoo na Furaha. Aidha, matawi yote ya benki za biashara zilizopo Zanzibar pia zinaendelea kutoa huduma ya kubadilisha fedha.

**(i) Hali ya Upatikanaji wa Dola ya Marekani**

**67.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23, nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania zilikumbwa na upungufu wa Dola ya Marekani. Changamoto hii ilisababishwa na mambo manne makubwa.

i. Vita vinavyoendelea nchini Ukraine ambavyo vilisababisha kupanda kwa bei za bidhaa na huduma duniani, hivyo kuongeza mahitaji ya Dola ya Marekani, ambayo ndiyo sarafu kuu katika biashara ya kimataifa;
ii. Sera ya Fedha ya Marekani, ambayo ilijielekeza kwenye kupandisha riba, hali iliyosababisha wawekezaji wengi kuelekeza mitaji yao Marekani na kusababisha upungufu wa dola kwenye nchi nyingine;Kufunguka kwa shughuli za kiuchumi baada ya athari za UVIKO-19, jambo lililoongeza mahitaji ya Dola za Marekani ukilinganisha na kiasi kilichopo kwenye masoko ya fedha;
iii. Mabadiliko ya tabia nchi, yaliyosababisha kupunguza uzalishaji hasa kwa nchi zinazoendelea na kuongeza mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kutumia dola ya Marekani. Kufuatia hali hiyo, washirika wetu wa maendeleo waliamua kuelekeza fedha zao kupambana na mabadiliko hayo katika nchi zao au nchi chache zaidi na hivyo kusababisha nchi nyingi zinazoendelea kushindwa kuzipata kutokana na masharti magumu yaliyofungamanishwa na upatikanaji wake.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa tunakabiliana na changamoto hii, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeamua kuchukua hatua mahsusi za muda mfupi, wa kati na

mrefu. Miongoni mwa hatua hizo ni kuweka mkakati wa kuongeza uzalishaji ili kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Aidha, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imekusudia kuhuisha Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji Wanaozalisha Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (Export Credit Guarantee Scheme). Sambamba na hayo, Benki Kuu itaendelea kutekeleza Sera ya Fedha itakayosimimia utulivu wa bei, uthibiti wa sekta ya fedha, kuchochea ukuaji wa uchumi, na kuhakikisha kuwa biashara katika soko la jumla la fedha za kigeni (Interbank Foreign Exchange Market) inakuwa yenye ushindani na tija zaidi.

**(ii) Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni Nchini**

69. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliagiza kupitia upya tathmini kuhusu uendeshaji wa maduka ya kubadilisha fedha (Bureau De Change) kuwekezesha na kurahisisha biashara hiyo hapa nchini. Hadi Mei 2023, Serikali ilikuwa imetoa leseni kwa maduka ya kubadilishia fedha za kigeni yapatayo 8 yenye matawi 36, ambapo matawi 24 yamefunguliwa Tanzania Bara na matawi 12 yamefunguliwa Zanzibar. Vile vile, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kukamilisha maombi ya maduka matatu ambayo yamewasilisha maombi hivi karibuni na kuendelea kuhamasisha Mabenki kuingiza Mashine za Kubadilishia Fedha (Forex ATM). Aidha, Benki Kuu inaendelea kupokea, kuchambua na kutoa leseni kwa Wamiliki wanaokidhi vigezo vilivyopo ili kurahisisha upatikanaji wa fedha za kigeni karibu na maeneo ya makaazi zu bishara za wananchi.

70. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Serikali zetu zitashirikiana kufanya mapitio ya Kanuni za Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya Mwaka 2019, kwa lengo la kurekebisha masharti yaliyopo kwa sasa ili kupanua wigo wa utoaji wa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni. Pamoja na masuala mengine, mapitio hayo yanatarajia kuanzisha madaraja ya maduka hayo kulingana na kiwango cha mtaji ambacho kinaweza kukidhi maeneo

yenye wateja wengi na wachache kwa makampuni yanayomilikiwa na wazawa au wawekezaji wageni watakaofungua biashara ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni.

71. **Mheshimiwa Spika,** mapitio hayo yanalenga pia kuweka utaratibu utakaowezesha hoteli za kitalii nchini kutoa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni kwa wateja wao, ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma hii na hivyo kuchangia utatuzi wa changamoto ya soko lisilo rasmi la kubadilishia fedha za kigeni nchini (black-market). Aidha, Serikali itaendelea kujenga mazingira rafiki na wezeshi kwa wafanyabishara wanaoendesha maduka ya kubadilishia fedha za kigeni; kutoa elimu kwa umma ili kudhibiti changamoto ya soko lisilo rasmi; na kuwezesha wafanyabishahara kusogeza huduma hizo kwenye maeneo yenye uhitaji.

- **Amana**

72. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2023, amana katika benki zilizopo Zanzibar ziliongezeka hadi kufikia TZS 1,640.0 bilioni ikilinganishwa na TZS 1,596.00 bilioni zilizokuwepo robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2022. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ilikuwa na asilimia 51.8 ya amana zote; ikifuatiwa na benki za CRDB, National Microfinance Bank (NMB), na ABSA ambazo kwa pamoja zilizochangia asilimia 28.0 ya amana zote.


- **Mikopo**

73. **Mheshimiwa Spika,** mikopo ni sehemu kubwa ya rasilimali za benki na chanzo chake kikubwa ni amana za wateja. Uchambuzi wa mikopo unaonyesha kuwa kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 thamani ya mikopo iliyotolewa ilifikia TZS 2,607.6 bilioni, ambayo ni ongezeko la asilimia 28.2 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka uliotangulia. Mikopo binafsi (ambayo zaidi inalenga wafanyakazi wa muda mrefu au wenye mikataba) ilichukua zaidi ya nusu (asilimia 52) ya mikopo yote iliyotolewa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023. Hii ilifuatiwa na sekta za biashara

na utalii zilizopata wastani wa asilimia 11.3 kila moja. Mikopo kwa sekta ya kilimo iliongezeka hadi kufikia asilimia 5.8 ikilikinganishwa na chini ya asilimia 1 iliyopata katika kipindi kama hicho mwaka uliopita.

74. **Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza wigo wa matumizi ya Sekta ya Fedha, kwa mwaka wa fedha 2023/24 Serikali inatarajia kutunga Sheria ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha pamoja na kanuni zake; kuanzisha bidhaa na huduma mpya katika Benki ya Kiislamu zitakazovutia zaidi wateja; na kuboresha huduma za mawakala ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kibenki.

**Sekta zilizofaidika na mikopo kutoka Benki**




***Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania*

- **Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.**

75. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwepo kwa baadhi ya wanachama wa Mifuko mengineyo ya Tanzania, Mfuko wetu wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ndio ambao umechukua sehemu kubwa ya soko la Zanzibar. Hadi kufikia mwezi Machi 2023, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) umeshasajili wanachama 119,277 ikiwa na ongezeko asilimia 9 ikilinganishwa na wananchama 108,697 waliokuwepo Machi, 2022. Mfuko umefanya malipo ya pencheni ya TZS 17.00 bilioni kwa wastaafu 11,620 ambapo ilikadiria kulipa TZS 13.00 bilioni kwa wanachama 10,790. Mfuko umefanya marejesho

ya TZS 3.57 bilioni kwa wanachama 161. Kadhalika, hivi karibuni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Zanzibar utaanzisha Huduma mpya ya Fao la Kuumia Kazini (Employment Injury Benefit) kwa lengo la kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Uwekezaji, Mfuko unaendelea kuwekeza ndani ya Zanzibar ili kuhakikisha rasilimali zinazozalishwa na Mfuko zinatumika kuwanufaisha Wazanzibari. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mfuko utaendelea kuwekeza katika maeneo ya Kituo cha Mabasi Kijangwani ambapo Mkandarasi tayari ameshapatikana na anatarajiwa kuanza kazi na Mradi huo kukamilika ndani ya miezi kumi. Aidha, Mfuko umeshawekeza katika ujenzi wa Maegesho ya Magari Malindi ambapo kazi hiyo inafanywa na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) na matarajio ni kuwa ujenzi huo utakamilika ndani ya miezi 12. Mfuko pia unaendelea na hatua za Ujenzi Nyumba za Bei Nafuu Viwanja vya Magereza - Mombasa na Ujenzi wa eneo la Michezo na Biashara Mbweni.

- **Sekta Ndogo ya Bima**

77. **Mheshimiwa Spika,** hali ya masoko ya Bima kwa upande wa Zanzibar kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 imeimarika kwa ukuwaji wa biashara ya bima kufikia asilimia 195 na ongezeko la watoa huduma za bima kufikia Makampuni ya bima kumi na tano (15) hapa Zanzibar. Jumla ya mikataba 54,284 yenye thamani ya TZS 37.7 bilioni imeandikishwa, ambapo makusanyo ya kipindi cha Julai 2021 – Machi 2022 yalikua TZS 12.8 bilioni. Kwa upande wa malipo ya fidia umejitokeza upungufu, kutoka TZS 5.7 billion kwa kipindi kama hicho kulichoishia Machi 2022 hadi TZS 2.7 billion kufikia Machi 2023 sawa na upungufu wa asilimia 53 ambapo wahanga 2,144 walilipwa fidia.

78. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2023, soko la Bima la Zanzibar limesajili jumla ya makampuni ya Bima 15 yakiwemo mashirika ya Bima ya Serikali (ZIC na NIC), Madalali wa Bima

wanne (4), Mawakala wa Bima 71 Mabenki Wakala wa Bima Sita (6) na mkadiria hasara mmoja (1). Jumla ya njia mpya nne (4) za usambazaji wa bidhaa za Bima zimeanzishwa ikiwa ni pamoja na: Benkiwakala wa Bima (Bancassurance); Bima ya Takaful (Takaful Operators); Utoaji Huduma za Bima Kidijitali (Insurance Digital Platforms) na Mfumo wa Maafisa Wauza Bima (Sales Force Executives); Uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa bima kati ya TIRA na Mamlaka zingine za Serikali. Hatua nyengine iliyochukuliwa ni kuanzishwa kwa Muungano wa Kampuni za Bima za Utoaji wa Bima za Mafuta na Gesi (Oil and Gas Consortium).

**Taasisi zinazotoa Huduma Ndogo Ndogo za Kifedha.**

79. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya vyama vya ushirika vilivyosajiliwa ni 1,822 (Unguja 1,036; Pemba 786), SACCOS 2 na vyama vya uzalishaji na utoaji wa huduma 1,820. Aidha, hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya taasisi sita (6) zimepatiwa ruhusa (no objection) ya kufanyakazi za huduma ndogo ndogo za kifedha Zanzibar ambapo lengo ni kusajili vyama 300 (Unguja; 200, Pemba 100). Utekelezaji wa zoezi hili umeongezeka zaidi ya mara mbili ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana ambapo Idara ilisajili jumla ya vyama 914.

**g) Sekta ya Nishati ya Umeme**

80. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuimarisha nishati ya umeme ambapo hadi kufikia Mwezi wa Machi, 2023 jumla ya uniti 430,252,267.72 kWh zimeuzwa kati ya 404,760,728.00 kWh zilizopangwa sawa na asilimia 106 ya mauzo na kupelekea makusanyo ya TZS 117,583,679,018.17 ambayo pia yamejumuisha na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

81. **Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya umeme (power consumption) yameendelea kukua na kuongezeka kwa wastani wa Megawati kumi na tano (15MW) baina ya mwaka 2021 hadi 2023. Mahitaji ya

juu ya umeme (peak demand) kwa upande wa Unguja yamefikia megawati 104.9 (matumizi katika waya wa megawati 100 yamefikia megawati 83, na waya wa megawati 45 yalifikia megawati 21.9) sawa na asilimia 72 ya uwezo wa waya mbili zilizopo yaliyofikiwa tarehe 31 Januari 2023. Kwa upande wa Pemba mahitaji ya juu ya umeme ni megawati 12 (12MW) sawa na asilimia 60 ya uwezo wa waya unaotumika hadi sasa wa megawati 20.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** kutokana na Zanzibar kutegemea umeme kutoka Tanzania Bara ipo haja ya kuwa na njia mbadala ya upatikanaji wa nishati hiyo, ili kuimarisha uhakika wa upatikanaji wa huduma hiyo. Hali hii inatokana na ukuaji wa sekta za kiuchumi na kijamii kunakosababishwa na ukuwaji wa sekta ya utalii, viwanda na biashara, na kuongezeka kwa idadi ya watumiaji wa umeme nchini.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) imeendelea kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kupanua mtandao wa usambazaji umeme kwa kiwango cha Kilovolti 33 na kilovolti 11. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya urefu wa mtandao wa kusafirisha umeme umefikia kilomita 1,645 sawa na ongezeko la asilimia 18.9 ikilinganishwa na kilomita 1,383 zilizokuwa zimefikiwa mwezi Machi, 2022.

### h) Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

**84.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 ili kufikia dhamira zilizowekwa kupitia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050. Uwezeshaji wananchi kiuchumi ni miongoni mwa mikakati mahsusi inayotekelezwa kwa lengo la kuinua kipato cha mwananchi, mjasiriamali na mfanyabiashara kwa kuwawezesha kwa kuwapa mafunzo, mikopo na masoko ya bidhaa zinazozalishwa na Wajasiriamali. Hadi kufikia Machi 2023, Serikali imefanikiwa kutoa mikopo 2,177 yenye thamani ya TZS 14.03 bilioni ambapo Unguja zimetolewa TZS 9.34 bilioni na Pemba zimetolewa TZS 4.69 bilioni

mikopo hiyo imewanufaisha Wajasiriamali 8,311 (Unguja 5,301 na Pemba 3,010). Kupitia Mfuko "Inuka" unaosimamiwa kwa pamoja kati ya Serikali na Benki ya CRDB, mikopo iliyotolewa hadi sasa imefikia TZS 17.97 bilioni ambayo imewafikia wanufaika 18,489 wakiwemo 7,050 wanaume na 11,439 wanawake. Kati ya hao, 37 ni wanufaika wenye mahitaji maalum.

85. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kupitia Sheria Nambari 2 ya Mwaka 2022 ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeunganisha Mifuko ya Uwezeshaji na mifuko mengine kama vile Mfuko wa Khalifa ili kuweza kunufaisha wananchi walio wengi zaidi. Taasisi hii imeshaunganishwa na SMIDA ili kuwaunganisha wajasiriamali na kuleta urahisi katika usimamizi wa sekta hii. Hivyo, kwa mwaka 2023/2024 Serikali imetenga TZS 1.19 bilioni kwa ajili ya uendeshaji wa taasisi hii, ambapo matarajio ni kupata maendeleo chanya kwa Wajasiriamali waliopo nchini.

### i) Sekta ya Uwekezaji

86. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuweka mazingira mazuri ya kisera na kisheria ili kuimarisha uwekezaji wa ndani na nje ambao utaweza kuongeza pato la taifa, kukuza ajira, uchumi wa nchi pamoja na kuleta maendeleo endelevu yatakayo imarisha ustawi wa wananchi bila ya kuharibu mazingira, silka, mila na tamaduni nzuri za Wazanzibari. Serikali kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) hadi kufikia mwezi Machi mwaka wa fedha 2022/2023 imefanikiwa kusajili miradi ya uwekezaji 74 ikilinganishwa na usajili wa miradi 73 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ya uwekezaji. Hadi kufikia Machi, 2023 miradi hiyo imetengeneza mtaji wa Dola za Kimarekani 444,977,054. Miradi hii imetengeneza jumla ya ajira 2,228.

87. **Mheshimiwa Spika;** katika kufanikisha uwekezaji ndani ya visiwa vidogo vidogo ambapo taratibu za kuanza uwekezaji katika visiwa vidogo vidogo zimeanza, jumla ya visiwa vitatu (Changuu, Bawe na Pamunda) vimeanza ujenzi wa maneo yao ya uwekezaji. Kwa

mwaka ujao wa fedha 2023/2024 Mamlaka inatarajia kupokea na kusajili miradi ipatayo 100 ambayo itatengeneza mtaji wa dola za Kimarekani zipatazo milioni 500 na kuleta ajira zipatazo 2,000 kwa wananchi.

**j) Sekta ya Usafirishaji**

**88.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Usafirishaji ni miongoni mwa Sekta muhimu katika kukuza uchumi wa nchi. Sekta hii inajumuisha usafiri wa baharini, usafiri wa nchi kavu na usafiri wa anga. Kwa upande wa usafiri wa baharini tayari Serikali inaendelea na mikakati ya kuendelea na uwekaji wa miundombinu rafiki ili kuruhusu Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani ambapo kwa sasa imeanza kujenga Barabara zenye urefu wa kilomita 12 katika eneo la Bandari ya Mangapwani kama zilivyoainishwa ndani ya Mpango Mkuu wa Bandari hiyo (Mangapwani Port Master Plan) pamoja na kupeleka miundombinu ya maji na umeme.

**89.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuimarisha Bandari ya Malindi kwa kuchimba mchanga katika Gati nambari 3 ili kuongeza kina cha maji hadi kufikia mita sita (6) kwa ajili ya kupata eneo jengine la kuegeshea meli, kukamilisha ujenzi wa Bandari Kavu (ICD) katika eneo la Bwawani lenye ukubwa wa mita za mraba 4,000, eneo ambalo lina uwezo wa kuhifadhi makontena 320 pamoja na kulifanyia matengenezo eneo la Maruhubi lenye ukubwa wa mita za mraba 10,000 lenye uwezo wa kuhifadhi makontena matupu zaidi ya 1,200 ili kupunguza msongamano wa makontena katika bandari hiyo. Vilevile, Serikali inaendelea kuimarisha Bandari ya Mkoani kwa kujenga eneo la kuhifadhia makontena lenye mita za mraba 4,200, kukamilisha matengenezo ya njia itakayotumika kupitishia magari na vitendea kazi pamoja na kujenga upya njia ya waenda kwa miguu kwa lengo la kuongeza usalama wa abiria wanaondoka na wanaowasili katika bandari hiyo. Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini (Micheweni) kwa kujenga gati yenye urefu wa mita 45 na upana wa mita 20 ili kurahisisha huduma za usafiri baina ya Pemba, Tanga

na Mombasa. Bandari hiyo itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli zenye uzito GRT (Gross Rated Tonnage) 2000. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga jumla ya TZS 20.00 Bilioni kwa ajili ya kuimarisha usafiri wa baharini.

90. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Usafiri wa Anga, Serikali kupitia Mpango wa Uimarishaji wa Viwanja vya Ndege imeanza kufanya Upembuzi Yakinifu wa Jengo la abiria namba 4 (Terminal 4) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume pamoja na kuendelea maandalizi ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kwa Mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali inatarajia kutumia TZS 160.00 bilioni kwa ajili ya Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba.

91. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa usafiri wa barabara, Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ya Wete – Chake yenye urefu wa km 22.1, Ujenzi wa Barabara za Ndani zenye urefu wa kilomita 275.9, Ujenzi wa Barabara za Mjini zenye urefu wa kilomita 100.9 pamoja na maandalizi ya Ujenzi wa Barabara ya Tunguu – Makunduchi (km 48.5), Fumba – Kisauni (km 12) na Mkoani – Chake Chake (km 48) ambayo inategemewa kuanza hivi karibuni. Pia Serikali itaanza na ujenzi wa barabara nyengine kuu zenye Urefu wa kilomita 277 Unguja na Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga jumla ya TZS 373.54 bilioni kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya Barabara Unguja na Pemba.

### k) Sekta ya Mawasiliano

92. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hichi, Sekta ya Mawasiliano ni muhimu sana katika maisha ya kawaida kutokana na kukuwa kwa teknolojia na kukuza uchumi wa nchi. Miundombinu bora ya mawasiliano huzidisha ufanisi katika Nyanja mbalimbali za Maisha yetu ya kawaida ikiwemo kurahisisha upatikanaji wa huduma za usafirishaji, huduma za fedha, usambazaji wa umeme, huduma za afya, na huduma nyenginezo ambazo kwa namna moja au nyengine zinasaidia kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla.

**93.** **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha 2022/2023, Zanzibar imepitia kipindi kizuri cha ukuaji wa kiuchumi uliosababishwa na ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano. Mafanikio ya ukuaji wa kiuchumi hapa Zanzibar yametokana na juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza sekta ya Mawasiliano kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya kimkakati ya Mawasiliano ikiwemo kukamilisha mradi wa ujenzi wa Minara 42 ya Mawasiliano Unguja na Pemba kwa kushirikiano Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), kuziunganisha na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Taasisi mbali mbali za Serikali Unguja na Pemba pamoja kuimarisha kituo cha kutunzia taarifa (Data Center) ili kutoa huduma bora za mawasiliano hapa Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga TZS 5.9 Bilioni kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya mawasiliano Zanzibar.

**l) Sekta ya Elimu**

**94.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Elimu ni miongoni mwa Sekta za vipaumbele vya juu vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hii ni kutokana na mchango mkubwa wa sekta hii katika kuzalisha wataalamu wa fani mbali mbali ambao wana mchango mkubwa wa kuliletea maendeleo Taifa letu kiuchumi, kisiasa na kijamii. Sekta ya elimu imekuwa ikiimarika siku hadi siku hasa katika miundombinu, uandikishaji na ufaulu wa wanafunzi katika kiwango cha divisheni ya kwanza unaongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mwaka 2022/2023, Serikali imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Skuli 10 za ghorofa Unguja na Pemba zikiwemo skuli 7 za msingi katika maeneo ya Kidongo-chekundu, Kwabitihamrani, Mwanakwerekwe na Jendele kwa Unguja na skuli za Mwambe, Kwale na Pujini kwa upande wa Pemba na Skuli 3 za Sekondari katika maeneo ya Bweleo, Pujini na Makangale. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa skuli 5 za Sekondari Unguja na Pemba katika maeneo ya Mtopepo, Mfenesini, Gamba, Mwembeladu na Kifundi. Aidha, jumla ya maabara 10 za sayansi zimekamilika katika skuli za Fukuchani,

Tumbatu, Bumbwini, Jendele na Machui kwa Unguja na maabara za Uondwe, Chanjamjawiri, Wambaa, Chambani na Shumba. Aidha, Serikali tayari imeshaandaa Mtaala mpya wa umahiri utakaotumika katika ngazi ya Elimu ya Maandalizi na Elimu ya Msingi. Jumla ya walimu 8,936 wa skuli za Serikali na binafsi Unguja na Pemba wameshapatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mtaala mpya.

95. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha masomo ya Hesabati, Sayansi na Kiingereza kwa kuwapatia mafunzo ya Mtaala wa Umahiri (Competence Based Curriculum) ili kuongeza viwango vya ufaulu katika skuli za Sekondari. Kwa upande wa Elimu ya Juu, Serikali imeongeza idadi ya mikopo kwa wanafunzi. Hadi Machi 2023, wanafunzi waliopatiwa mikopo ni 4,875 ikiwa ongezeko la wanafunzi wapya 1,815 na 3,060 wanaendelea na masomo. Kwa mwaka 2023/2024, Serikali imetenga TZS 20.0 bilioni kwa ajili ya Bodi ya Elimu ya Juu ya Zanzibar ili kuongeza wigo wa kuwapatia mikopo wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu.

96. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kukamilika Ripoti ya Mageuzi ya Sekta Elimu, Serikali itaendelea na mpango wa utekelezaji wa mageuzi hayo. Kwa sasa, Serikali inaifanyia mapitio Sera ya Elimu pamoja na Sheria ya Elimu ili kwenda sambamba na mageuzi ya elimu itakayoiwezesha kufikia malengo mbali mbali ya Kitaifa na Kimataifa.

### m) Sekta ya Afya

97. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika huduma za afya zenye ubora na zinazowafikia wananchi wote ili kuboresha afya zao. Serikali inatambua umuhimu wa afya bora kwa wananchi wake kwani afya bora ni rasilimali muhimu kwa maendeleo. Maendeleo ya nchi yetu yataletwa na wananchi wenye afya na wenye uwezo wa kuzalisha mali. Katika kuhakikisha kuwa wananchi wana afya bora, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa huduma za afya kwa kuzingatia sera na miongozo iliyopo.

98. **Mheshimiwa Spika,** huduma za afya nchini zimeendelea kutolewa kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na mabadiliko endelevu yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya nane chini ya uongozi wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa BLM katika Sekta ya hii kwa lengo la kuleta uwiano katika upatikanaji wa huduma bora za afya mijini na vijijini. Kiujumla, hali ya afya ya wananchi wengi imeendelea kuwa ya wastani licha ya changamoto zinazoendelea kujitokeza kutokana na matumizi ya yasiyo sahihi ya vyakula, bidhaa zisizo na viwango na uharibifu wa mazingira ambayo huleta athari hasi katika afya ya mwanadamu. Hali hii imesababisha kupungua kwa kasi ya kufikia malengo yanayotarajiwa. Serikali inaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kulinda afya zao na kutumia huduma za afya zinazotolewa na Serikali.

99. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia hilo, kwa mwaka 2022/2023, Serikali imekamilisha ujenzi wa Hospitali kumi za Wilaya na moja ya Mkoa na tayari baadhi zimeshaanza kutowa huduma ikiwemo: Hospitali ya Wilaya ya Kusini Kitogani na Hospitali ya Wilaya ya Micheweni. Hospitali ya Wilaya ya Mjini iliyojengwa Chumbuni, Hospitali ya Wilaya Magharibi "B" iliyojengwa Magogoni, Hospitali ya Wilaya Magharibi "A" iliyojengwa Mbuzini, pamoja na Hospitali ya Mkoa iliyojengwa Lumumba zinaendelea kuwekewa miundombinu na kufungwa mashine na vifaa tiba na matarajio ya Serikali ni kuanza kazi mapema Mwaka 2023/2024. Aidha, Serikali imeshaajiri wafayanyakazi 937 kwa ajili kutoa huduma katika vituo hivyo. Serikali pia itaendelea kushirikiana na Sekta binafsi zinazoekeza katika kutoa huduma ya afya ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Hadi, kufikia Machi 2023, Zanzibar kuna vituo 171 vinavyotoa huduma za afya za awali na Hospitali 4 ikiwemo: Al-Rahma, Tawaakali, Amal (iliyoko Chake Chake Pemba) na Ampola Tasakhtaa maarufu kama Global Hospital.

100. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza yakiwemo maradhi makuu kama vile malaria, kifua kikuu na UKIMWI pamoja na kuimarisha huduma za Mama na Mtoto ili kupunguza vifo.Katika kupambana na changamoto hiyo Serikali itatumia mikakati ifuatayo:

i. Kuendelea kuhamasisha kina mama kuhudhuria katika vituo vya afya kwa vipindi vinane (8) vya ujauzito,
ii. Kuwahamasisha kufika mapema hospitali wakati kujifungua ili kupatiwa huduma stahiki na kuweza kugundua matatizo mapema,
iii. Kupatiwa elimu ya Lishe na matumizi bora ya vyakula,
iv. Kupatiwa virutubisho vya madini ya chuma ili kusaidia kuongeza damu,
v. Kushajiisha matumizi ya uzazi wa mpango,
vi. Kuimarisha huduma za watoto njiti kwa kujenga vituo vya "neonatal care" ndani ya hospital zote,na
vii. Kuwajengea uwezo wahudumu wa kuweza kuwasaidia watoto kupumua (helping babies breath) ambapo wahudumu 200 wameshasomeshwa jinsi ya kutoa huduma hiyo.

101. **Mheshimiwa Spika,** Serikali, imekamilisha matayarisho ya Mfuko wa Huduma za Afya (Zanzibar Health Service Fund) ukiwa na lengo la kufikia upatikanaji wa huduma bora za afya za uhakika na endelevu kwa wananchi na wakaazi wote wa Zanzibar. Kwa mwaka 2023/2024, Serikali imetenga jumla ya TZS 239.15 bilioni ikiwa ni asilimia 8.42 kwa ajili utoaji wa huduma za afya nchini.

### n) Upatikanaji wa Maji Safi na Salama

102. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua kuwa maji ni sehemu ya haki ya msingi ya binadamu. Sekta ya maji inakumbwa na ongezeko la mahitaji ya huduma hiyo kunakochochewa na ongezeko la idadi ya watu, kukua kwa miji pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo uwekezaji na utalii, mabadiliko ya tabianchi, uvamizi wa vianzio vya maji, uchakavu wa miundombinu ya maji na mwitikio mdogo wa wananchi kuchangia huduma ya maji, vyote hivyo vinaipa changamoto kubwa sekta ya maji. Serikali itaendelea na mikakati ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi Mijini na Vijijini inafikia zaidi ya asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, Serikali inaendelea kujenga, kukarabati, kusambaza

mitandao ya maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji Nchini.

103. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2023 hali ya uzalishaji maji nchini imeendelea kuimarika ambapo kwa ujumla wastani wa uzalishaji wa maji umefikia asilimia 67 kwa Unguja na Pemba ikilinganishwa na asilimia 56 iliyofikiwa mwezi Machi, 2022. Aidha, mahitaji ya maji nchini yameendelea kukua ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2023 mahitaji ya maji yamefikia lita 240,465,120 kwa siku na uzalishaji ni lita 146,926,338 kwa siku hivyo kupelekea kuwa na upungufu wa lita 93,538,782 kwa siku.

104. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia kukamilika kwa utekelezaji wa miradi mbali mbali ya Sekta ya Maji nchini, kiwango cha uzalishaji maji kinatarajiwa kuongezeka zaidi na kufikia wastani wa asilimia 75 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2023. Kukamilika kwa miradi ya maji ambayo inaendelea kutekelezwa katika kipindi hichi kutanufaisha wanawake takriban 355,523 na hivyo,kuwezesha wanawake hawa kujishughulisha na shughuli nyengine za kiuchumi na uzalishaji zaidi katika muda ule ambao wanaoutumia katika kutafuta maji.

### o) Michezo, Sanaa na Utamaduni

105. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya michezo, Serikali imeendelea kuimarisha viwanja mbali mbali vya michezo katika visiwa vya Unguja na Pemba. Viwanja ambavyo vinaendelea kukarabatiwa hadi sasa ni pamoja na viwanja viwili vya nje na viwanja viwili vya indoors ikiwa ni pamoja na kuanza ukarabati mkubwa wa Uwanja wa Aman. Serikali, kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) imekamilisha ukarabati wa Kiwanja Cha Michezo katika eneo la Matumbaku ambacho kitatumika kwa michezo kadhaa.

106. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Zanzibar ilishiriki mashindano ya Kikanda na Kimataifa kupitia michezo mbali mbali ikiwemo Mchezo wa Kabadi, Mchezo wa Judo, mchezo wa riadha na mpira wa pete ambapo jumla ya medali 36

zimepatikana. Katika sanaa, vikundi vipatavyo 43 vimesajiliwa na wasanii wameendelea kushiriki katika mashindano mbali mbali ya utamaduni ndani na nje ya Zanzibar.

### p) Utulivu, Amani na Utawala Bora

107. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa utawala bora hapa nchini. Hatua mbali mbali zimechukuliwa ikiwemo: Kuimarishwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kujengewa uwezo kwa Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi, kuimarishwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, pamoja na kuimarisha mifumo ya Mahkama ni kielelezo tosha kwamba Serikali inaendelea kulipa kipaumbele suala la utawala bora kuwa ni msingi wa maendeleo ya jamii na uchumi wetu.

108. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na mambo mengine, Serikali imepandisha madaraja viongozi wa taasisi za usimamizi wa utawala bora pamoja na kuimarisha vitendea kazi ili kuweka mazingira mazuri ya utendaji wao. Katika kukabiliana na vitendo vya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Ofisi zetu za ZAECA zimefunguwa majalada 31 ya watendaji wanaotuhumiwa kwa kesi mbali mbali za uhujumu uchumi, na kwaupande wa udhibiti maadili ya viongozi asilimia ya viongozi waliojaza fomu za tamko la mali na madeni nakurejesha katika Ofisi ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeongezeka.

109. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa, Zanzibar inaendelea kuwa tulivu kisiasa, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameunda na kuizindua rasmi kamati ya maridhiano na kuunda kikosi kazi ambacho kitafanyia kazi mapendekezo mbali mbali ambayo yametolewa wakati wa mikutano ya vyama vya siasa. Lengo ni kuimarisha amani na utulivu nchini, hasa katika nyakati za kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu.

## I. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2023

110. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023 mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar unakwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050, ZADEP 2021-2026 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020. Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2023 kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kuongezeka kwa asilimia 30 ya uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kutoka watalii 548,503 kwa mwaka 2022 hadi watalii 713,053 mwaka 2023;

ii. Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara za mjini na vijijini, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani na ukarabati wa Bandari ya Malindi. Miradi mingine itakayochangia ukuaji wa uchumi ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama na ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila Wilaya;

iii. Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei ili kubakia kwa tarakimu moja;

iv. Kuongezeka kwa usimamizi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na matumizi ya Serikali;

v. Kuongezeka kwa hatua za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza miradi binafsi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje; na

vi. Serikali kuongeza utekelezaji na usimamizi wa Miradi ya Kimkakati.

vii. Kuimarika kwa hali ya amani na utulivu ndani ya nchi na nchi za jirani pamoja na zile tunazofanya biashara nazo.

## J. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

111. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa za kuweka mfumo wa kodi uliotulivu na wenye kutabirika, kushajihisha

ulipaji wa kodi kwa hiari, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali, na hivyo kuchochea kasi ya ukuaji wa Uchumi katika Sekta mbali mbali nchini.

112. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itaendelea kuchukua hatua kadhaa za kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hatua hizo zinazopendekezwa kuchukuliwa na Serikali ni zile zinazohusu marekebisho ya Sheria pamoja na zinazohusu kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi.

**a. Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya Mwaka 1998**

**i. Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Uuzaji wa Nyumba Nafuu (Affordable Housing Scheme)**

113. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kuimarisha makaazi ya Wananchi kwa kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Miradi ya Nyumba Nafuu zitakazokuwa na vigezo maalum vitakavyoainishwa katika Kanuni na Miongozo itakayotangazwa baadae na Serikali. Hatua hii inalenga kuimarisha makaazi bora kwa Wananchi pamoja na kupunguza gharama za ununuzi wa nyumba hizo.

**ii. Kutoa Unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) wakati wa Uingizaji wa Ndege, Injini za ndege, Vipuri na huduma za matengenezo zinazofanyika nchini**

114. **Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa wamiliki wa ndege kuhusu kutokusamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) wakati wa uingizaji wa Ndege, Injini za Ndege na Vipuri. Hali hii imepelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa Ndege kutokana na kutoruhusiwa kudai Ankara za Kodi (input tax) iliyolipwa wakati wa uingizaji wa vifaa. Hivyo, Serikali inapendekeza kutoa unafuu wa VAT kwa uingizaji wa Ndege, Injini za Ndege, Vipuri na huduma za matengenezo zinazofanyika nchini ili kuondoa changamoto hizo, kuongeza ujuzi wa huduma za ufundi

nchini, pamoja na kuongeza usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**iii. Kupunguza unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Asasi za Kiraia kutoka asilimia 75 hadi asilimia 50**

**115. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/24, Serikali inapendekeza kupunguza unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Asasi za Kiraia (NGO's) kutoka asilimia 75 hadi asilimia 50 ili kudhibiti utaoji wa misamaha ya kodi pamoja na kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Aidha, (NGO's) zitalazimika kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria husika, kulipa kodi pamoja kuchangia katika michango muhimu ikiwemo ZSSF. Hatua hiyo itakwenda sambasamba na uwasilishaji wa ripoti ya utekelezaji wa kazi kwa kipindi cha miaka miwili, pamoja na vyanzo vya mapato kutoka ndani na nje ya nchi wakati wa maombi ya msamaha husika.

**iv. Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Uingizaji wa "Green House" na vifaa vyake**

**116. Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa uingizaji wa "Green House" na vifaa vyake. Hatua hiyo inatarajiwa kuimarisha shughuli za kilimo cha kisasa, kuongeza uzalishaji, kupunguza uagiziaji wa chakula kutoka nje pamoja na kupunguza mfumko kazi ya bei nchini.

**v. Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Uingizaji wa Vifaa vya Umeme Unaotokana na Nishati Jadidifu (Renewable Energy).**

**117. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/24, Serikali inapendekeza kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa uingizaji wa Vifaa vya Umeme Unaotokana na Nishati Jadidifu (Renewable Energy) ili kushajihisha uwekezaji wa umeme nchini, pamoja na kuwa na nishati ya kutosheleza kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda nchini.

**vi. Kuongeza Kiwango cha Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka Mauzo Ghafi TZS 50 milioni hadi TZS 100 milioni kwa Mwaka**

**118. Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa vigezo vya mlipakodi kusajiliwa kuwa Wakala wa Ukusanyaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ni kuwa na mauzo ghafi ya TZS 50 Milioni kwa mwaka. Kiwango hicho kimepitwa na wakati na hakiendani na uchumi wa Zanzibar kwa sasa, ili kutoa fursa kwa walipakodi wadogo kujiimarisha sambamba na hatua ya Serikali ya kuwawezesha pamoja na kurahisisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kwa walipakodi wadogo na wa kati. Inapendekezwa kuongeza kiwango cha usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka mauzo ghafi TZS 50 milioni hadi TZS 100 milioni kwa mwaka.

**b. Marekebisho ya Sheria ya Mafunzo ya Amali Nam. 11 ya Mwaka 2008**

**i. Kupunguza Kiwango cha Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (SDL) kutoka asilimia tano (5) hadi nne (4)**

**119. Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu yaliyowasilishwa katika Baraza la Taifa la Biashara na Kongamano la Kodi kutoka kwa waajiri wa Sekta binafsi kuhusu uwepo wa viwango vikubwa vya Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (SDL). Aidha, hali hiyo imepelekea baadhi ya Wafanyabiashara kushindwa kutoa taarifa sahihi kwa kuhofia kutozwa kiwango kikubwa cha kodi. Hivyo, ili kuondoa changamoto hiyo, pamoja kuongoza ulipaji wa kodi wa hiari, Serikali inapendekeza kupunguza kiwango cha Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (SDL) kutoka asilimia tano (5) hadi asilimi nne (4).

**ii. Kuongeza Idadi ya Waajiriwa Kutoka Waajiriwa wanne (4) hadi watano (5) Wakati wa Utozaji wa Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (SDL)**

**120. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2023/24, Serikali inapendekeza kuongeza idadi ya waajiriwa kutoka waajiriwa wanne (4) hadi watano (5) wakati wa utozaji wa Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (SDL) ili kwenda sambasamba na mabadiliko ya uchumi wa Zanzibar.

**iii. Kuweka Utaratibu wa Uwasilishaji wa Ritani kwa Waajiri Wenye Wafanyakazi Chini ya Watano (5)**

**121. Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kuweka utaratibu wa kuwasilisha ritani kwa kila nusu mwaka kwa Waajiri wenye wafanyakazi chini ya watano (5) na wasiopungua wafanyakazi watatu (3). Hatua hii inalenga kumarisha usimamizi wa mwenendo wa uajiri katika Sekta Binafsi.

**c. Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015**

**i. Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa Nchini**

**122. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2023/24, Serikali inapendekeza kuanza kutoza Kodi ya Miundombinu kwa asilimia moja (1%) kwa uingizaji wa bidhaa nchini (importation) ili kuongeza ufanisi wa miundombinu nchini. Aidha, Kodi hiyo haitahusisha bidhaa za vinwaji vikali, Sigara na Tumbaku, ambapo tayari zinatozwa asilimia kumi (10%) ya kodi hiyo. Hatua hii inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 5.7 bilioni.

**ii. Kutoa unafuu wa Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa Nchini**

**113. Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kutoa unafuu wa kodi ya miundombinu kwa uingizaji wa bidhaa nchini kwa taasisi zifuatazo:-

i. Taasisi za Serikali ambazo zinahudumiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina;
ii. Miradi ya Washirika wa Maendeleo (Donor Funded Project);

iii. Wazalishaji waliosajiliwa (Registered Manufacturer) kwa uingizaji wa malighafi, pembejeo za viwandani na vifungashio;
iv. Umoja wa Mataifa na Taasisi zake; na
v. Ubalozi.

**iii. Kurudisha Kiwango cha Awali cha TZS 100 ya Kodi ya Miundombinu kwa Lita ya Mafuta ya Dizeli na Petroli**

**114. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2023/24, Serikali inapendekeza kurudisha kiwango cha awali cha TZS 100 kwa lita ya mafuta ya Dizeli na Petroli kutoka TZS 50 ya kiwango cha sasa. Aidha, hatua hiyo haitaongeza gharama za ununuzi wa bidhaa hiyo kwa Wananchi kutokana na fedha hizo zitaingizwa katika Mfuko wa Uhimilivu wa Uchumi (Economic Stabilization Fund) ili kuendelea kutoa kufidia katika bidhaa hiyo iwapo gharama za ununuzi zitapanda katika soko la Dunia au kupanda kwa gharama za usafirishaji. Hatua hii inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 8.9 bilioni.

**iv. Marekebisho ya Viwango Vya Kodi ya Miundombinu kwa Wageni Wanaolala Katika Hoteli za Zanzibar**

**115. Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikitoza USD 1 kama Kodi ya Miundombinu kwa Mgeni anayelala katika Hoteli za Zanzibar. Kiwango hicho kimepitwa na wakati na hakiendani na mabadiliko makubwa ya kiuchumi yanayoendelea na yanayohitajika hapa Zanzibar. Pia, kiwango hicho hakijazingatia mabadiliko ya kasi ya mfumko wa bei na thamani ya ubadilishaji wa fedha za kigeni. Hivyo, inapendekezwa kama ifuatavyo:-

i. Dola za Marekani 5 kwa Mgeni anayelala katika Hoteli zenye hadhi ya nyota tano na nne (Five Stars Hotel & Four Stars Hotel);
ii. Dola za Marekani 4 kwa Mgeni anayelala katika Hoteli zenye hadhi ya nyota tatu au mbili (Three Stars Hotel & Two Stars Hotel); na
iii. Dola za Marekani 2 kwa Mgeni anayelala katika Hoteli zenye

hadhi ya nyota moja na nyengine zote ambazo hazijapewa hadhi ya nyota. Hii pia itahusisha kwa wageni wanaolala nje ya hoteli (AirBnB & Home Stays).

**d. Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa No. 8 ya mwaka 2017 Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa "Electronic Cigarettes" na "Shisha"**

116. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na kuongezeka kwa mutumizi ya"Electronic Cigarettes" na "Shisha" kwa vijana wetu ambao ndio nguvu kwa Taifa. Aidha, ongezeko hilo limetokana na kutokutozwa kodi kwa bidhaa hizo. Hivyo, inapendekezwa kuanza kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 30 kwa uingizaji wa "Electronic Cigarette" na "Shisha" ili kupunguza matumizi ya bidhaa hizo. Vile vile, kutakuwa na utaratibu maalum wa biashara hiyo kufanyika katika maeneo maalumu yatakayoratibiwa na Taasisi husika. Hatua hii inakwenda sambamba na upigaji marufuku wa uuzwaji wa sigara kiholela na vibali vya uuzwaji wa bidhaa hiyo itatolewa katika maeneo maalumu na Mamlaka husika.

**e. Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Barabara Nam. 7 ya Mwaka 2003**

**Kuanza Rasmi Kusajili Vyombo vya Maringi Manne, Matatu na Mawili Vinavyotumia Nishati ya Umeme Badala ya Nishati ya Mafuta**

117. **Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya vyombo vya maringi mawili vinavyotumia nishati ya umeme badala ya nishati ya mafuta bila kusajiliwa. Hali hiyo inaleta changamoto ya kutambua mmiliki halisi wa chombo husika iwapo vitapata ajili au kutumika katika shughuli za kiuhalifu. Hivyo, Serikali inapendekeza kuanza rasmi kuvisajili vyombo vya Maringi Manne, Matatu na Mawili Vinavyotumia Nishati ya Umeme Badala ya Nishati ya Mafuta ili kudhibiti udhibiti, pamoja na kuongeza usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**f. Marekebisho ya Sheria ya Tozo la Petroli Nam. 7 ya Mwaka 2001**

**118. Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kurudisha viwango vya awali vya Tozo la Petroli, Tozo la Kuendeleza Barabara na Ada ya Usajili wa Njia kwa uingizaji wa mafuta ya Dizeli na Petroli kama itakavyoainishwa katika Jadweli hapo chini. Aidha, hatua hiyo haitaongeza gharama za ununuzi wa bidhaa hiyo kwa Wananchi kutokana na fedha hizo zitaingizwa katika Mfuko wa Uhimilivu wa Uchumi (Economic Stabilization Fund) ili kuendelea kutoa kufidia katika bidhaa hiyo iwapo gharama za ununuzi zitapanda katika soko la Dunia au kupanda kwa gharama za usafirishaji. Hatua hii inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 12.8 bilioni.

***Jadweli***

| Viwango vya Awali Vinavyopendekezwa Ikilinganishwa na Viwango vya Sasa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Dizeli | | Petroli | |
| S/N | Maelezo | Kiwango cha Awali | Kiwango cha Sasa | Kiwango cha Awali | Kiwango cha Sasa |
| 1 | Tozo la Petroli | 350 | 350 | 350 | 300 |
| 2 | Tozo la Kuendeleza Barabara | 100 | 100 | 100 | 70 |
| 3 | Ada ya Usajili wa Njia | 38 | 15 | 38 | 15 |

**g. Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 7 ya Mwaka 2017**

**Kuongeza Kiwango cha Presumptive Tax Scheme kutoka Mauzo Ghafi ya TZS 5 Milioni hadi TZS 100 Milioni**

**119. Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa wafanyabiashara kulipa kodi ya mapato inayokusanywa na TRA na Ushuru wa Stempu unaokusanywa na ZRA. Hali hii inaongeza gharama za uwajibikaji kwa mlipakodi, pamoja na kupunguza morali ya ulipaji wa kodi kwa hiari. Ili kuondoa changamoto hiyo, na kurahisisha biashara na ulipaji kodi wa hiari, inapendekezwa Kufuta Utozwaji wa Kodi unayokusanywa na

TRA na ZRA kwa mfanyabiashara mmoja badala yake kuanzisha Kodi Mpya itakayaitwa Ushuru wa Mauzo Ghafi (Turnover Duty) ambao utasimamiwa na kukusanywa na ZRA. Ushuru utalipwa na Wafanyabiashara wenye mauzo ghafi yanayoanzia TZS milioni 5 na yasiyozidi TZS milioni 100 kwa mwaka. Sambamba na hilo, Ushuru wa Stempu utabakia kutozwa katika Hati tu. Matarajio ya hatua hii, ni kuendelea kulipa kodi kwa hiari kwa kudai na kutoa risiti.

**h. Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi Nam. 7 ya Mwaka 2009**

**i. Kufuta Adhabu (Penalty) kwa Walipakodi ambao wameshindwa kulipa kodi kwa wakati**

120. **Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu sasa sheria za kodi zimekuwa zikitoza Adhabu (Penalty) na Riba (Interest) kwa Walipakodi walioshindwa kulipa kodi kwa wakati. Aidha, hali hiyo imepelekea Walipakodi kulimbikiza madeni ya kodi kutokana na kushindwa kulipa Adhabu (Penalty). Hivyo, Serikali inapendekeza kufuta Adhabu (Penalty) ili kuondoa changamoto hiyo, pamoja na kuongeza ulipaji wa kodi wa hiari.

**ii. Kuweka utaratibu kwa Wageni Wanaolala katika Hotel za Zanzibar Kuwasilisha "Check Out Report" wakati wa Kuondoka nchini**

121. **Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na changamoto ya muda mrefu kwa baadhi ya Hoteli kushindwa kuwajibika na sheria za kodi ikiwemo kutotoa taarifa sahihi za wageni waliolala katika hoteli zao na gharama walizolipia hivyo kupelekea upotevu mkubwa wa mapato ya kodi za Serikali.ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za wageni kwa mujibu wa sheria, inapendekezwa kuweka utaratibu utakaorahisisha uwasilishaji wa "Check Out Report" kwa wageni waliolala katika hoteli husika wakati wa kuondoka nchini. Muongozo wa utaratibu huo utatolewa na Mamlaka husika.

## K. VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MWAKA 2023/2024

122. **Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya mwaka 2023/2024 imejikita kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Miaka Mitano (ZADEP) (2021/22 – 2025/26); Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Dira ya Maendeleo ya 2050 inayokwenda sambamba na Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na mikakati mengine ya maendeleo ya Taifa, Kikanda na Kimataifa.

123. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ikiwa ni upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina nafasi kubwa katika kukuza uchumi wa Ukanda wa Afrika Mashariki. **Bajeti hii imelenga Kuinua Uchumi wa Wananchi wa Zanzibar na Kuimarisha Miundombinu ili Kuvutia Uwekezaji hapa Nchini.** Katika mwaka 2023/24, maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kugharamia miradi ya kielelezo inayoendelea; ulipaji wa pencheni kwa wastaafu kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa BLM aliyoyatowa Siku ya Wafanyakazi Duniani,(May Day) la kuwaongeza pencheni wastaafu wa SMZ pamoja na kuongeza Pencheni Jamii kwa asilimia 150, kulipa mishahara ya watumishi wa Umma pamoja na maposho maalum kwa wakuu wa divisheni na wakuu wa vitengo. Vile vile kwa mazingatio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Muda wa Kati (ZADEP) (2021/22 – 2025/26), Serikali inakwenda kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

### a. Kuendelea Kuimarisha Miundombinu ya Barabara

124. **Mheshimiwa Spika,** eneo hili litahusisha ujenzi wa barabara kuu, barabra za mjini, barabara za ndani na vijijini zenye urefu wa kilomita 782.1 kilomita ambazo zitagharimu jumla ya TZS 373.5 bilioni.
    i. Programu ya Ujenzi wa barabara kuu (Chake Chake - Mkoani km 43, Tunguu-Makunduchi km 48.5, Chake Chake – Wete km 22, Fumba - Kisauni km 12); ambapo ujenzi huo unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 206.3 bilioni;

ii. Programu ya ujenzi wa barabara za mjini kilomita 103.7; utatumia TZS 80.1 bilioni;
iii. Programu ya ujenzi wa barabara za ndani na vijijini kilomita 275.9. utatumia jumla ya TZS 44.0 bilioni; na
iv. Ujenzi wa Barabara Kuu 277 kilomita, unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 43.0 bilioni kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**b. Kuimarisha Huduma za Jamii**

**125. Mheshimiwa Spika,** eneo hili litahusisha sekta tofauti zinazohusiana na usambazaji wa huduma za jamii ikiwemo sekta elimu, afya, usambazaji wa huduma za maji sambamba na uimarishaji wa sekta ya michezo. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 serikali inatarajia kutumia jumla ya TZS 338.8 bilioni kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo:

i. Ukarabati wa Hospital ya Rufaa ya Mnazi Mmoja unakadiriwa kutumia TZS 10.00 bilioni ;
ii. Ujenzi na uimarishaji wa Nyumba za Madaktari TZS 20.00 bilioni;
iii. Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Elimu ikijumuisha: miundombinu ya skuli; maabara na nyumba za walimu; kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kujifunza na kufundishia; kuandaa walimu na mitaala mipya) inakadiriwa kutumia TZS bilioni 64.0 bilioni;
iv. Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji wa Maji Safi na Salama unakadiriwa kutumia TZS 77.5 bilioni;
v. Kuongeza usambazaji na kuunganisha umeme mijini na vijijini ikiwemo utekelezaji wa mradi wa ZESTA utatumia TZS 16.0 bilioni;
vi. Mradi wa kuimarisha ulinzi na usalama unakadiriwa kutumia TZS 20.00 bilioni;
vii. Ujenzi wa viwanja vya michezo unakadiriwa kutumia TZS 34.3 bilioni
viii. Mpango Shirikishi wa Kukuza Uchumi Zanzibar (Boost Inclusive Growth in Zanzibar- Big Z) unakadiriwa kutumia TZS 22.8 bilioni; na

ix. Ujenzi wa ofisi za Serikali za kutolea huduma unakadiriwa kutumia TZS 74.1 bilioni.

### c. Kuimarisha Uchumi wa Buluu

**126. Mheshimiwa Spika,** katika uimarishaji uchumi wa buluu serikali inalenga kukuza na kuimarisha matumizi endelevu ya bahari na kuwawezesha wajasiriamali kwa kuongeza thamani mazao ya baharini na kukuza mitaji yao. Kwa mwaka wa fedha 2023/24 Mradi huu utatumia jumla ya TZS 23.5 bilioni kwa fedha za Serikali

i. Ujenzi wa Bandari za uvuvi - Mangapwani 10.5 bilioni
ii. Ujenzi wa masoko na minada ya kisasa ya samaki katika maeneo ya Kama na Fungurefu kwa Unguja na Wete na Mkoani kwa Pemba 13.00 bilioni;

### d. Kuimarisha miundombinu ya Bandari na Viwanja vya ndege

**127. Mheshimiwa Spika,** lengo ni kuimarisha bandari na viwanja vya Ndege Unguja na Pemba ambavyo vitaweza kuhudumia wananchi pamoja na watalii. Kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 Mradi huu utatumia jumla ya TZS 180.00 bilioni.

i. Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, utatumia jumla ya TZS 160.00 bilioni; na
ii. Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani, utatumia jumla ya TZS 20.00 bilioni.

### e. Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Mapato yanayotokana na Utalii

**128. Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ina fursa ya kipekee katika anga za kitalii kutokana na jina, mandhari, umahiri, mazingira pamoja utamaduni wa watu wake. Maendeleo ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea kutokea, yanalenga pamoja na mambo mengine, kuhakikisha kuwa, upekee wa Zanzibar katika taswira ya kitalii unaleta tija ya kiuchumi pamoja na maendeleo ya watu wake.

129. **Mheshimiwa Spika,** changamoto kubwa iliyopo kwa sasa, ni kuwa ongezeko la watalii hapa Zanzibar haliakisi mapato yanayoingia Serikalini. Kwa mfano, baina ya mwezi wa Julai 2021 hadi Juni 2022, mapato ya utalii yaliyorikodiwa katika mifumo ya Serikali yalifikia TZS 69.89 bilioni na baina ya Julai 2022 hadi Machi 2023, mapato yaliyoingia katika Serikali kutoka vyanzo mbali mbali ya utalii yamefikia TZS 51.32 bilioni. Hivyo, Serikali itaendelea na jitihada za kuweka sera sahihi pamoja na mikakati ikiwemo mifumo ambayo itahakikisha uwepo wa uwiano madhubuti baina ya ongezeko la watalii na mapato ya Serikali yanayotokana na shughuli za utalii.

**f. Kulipa Amana za Wananchi waliyokuwa na Amana katika Benki ya FBME**

130. **Mheshimiwa Spika,** mnamo mwaka 2017, Benki Kuu ya Tanzania, ilisimamisha shughuli za biashara kwa iliyokuwa Benki ya FBME ambayo ilikuwa na makao yake makuu yake nchini Cyprus ilifungua tawi mjini Dar-Es-Salaam. Benki hii pia ilikuwa na Tawi hapa Zanzibar. Benki hii ilianza shughuli zake mnamo mwaka 2003. Mnamo mwaka 2014, Benki hii iliwekwa chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania na 2017, ikawa chini ya ufilisi wa Bodi ya Bima za Amana (DIB). Hadi inawekwa chini ya ufilisi, idadi ya wateja walikuwa ni 6,600 ambapo wateja wa Zanzibar ni 2,329. Kwa wateja wa Zanzibar, madai yao yalifikia TZS 20,508,503,194.08. Hata hivyo, kwa kuwa hadi sasa, kesi baina ya DIB na Mamlaka za Cyprus ambako pia kuna amana za FBME inaendelea, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeamua kulipa amana za wateja wa iliyokuwa FBME kwa upande wa Zanzibar. Serikali, itaanza mchakato huo, mara baada ya kukamilika taratibu ambazo itazitangaza baadae.

**g. Utaratibu wa Malipo ya Pencheni Jamii**

131. **Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo imetanguliwa kutangazwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeamua kuongeza Pencheni kwa kiwango cha asilimia 100 kwa wale wenye kiwango cha chini

cha pencheni. Serikali vile vile, itaanza kulipa ongezeko la pencheni jamii kutoka TZS 20,000 hadi TZS 50,000 kwa wazee wenye umri wa miaka 70+. Hata hivyo, kwa kuwa kumekuwa na ongezeko hili, pencheni jamii itaanza kulipwa kwa kutumia mifumo ya kibenki kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar. Tayari uhakiki umekamilika na taratibu zinaendelea kwa kuwafungulia wazee wote akaunti. Mawakala wa PBZ, Maafisa wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Maafisa wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto watashirikiana kwa pamoja katika kufanya malipo hayo.

**h. Uanzishwaji wa Benki ya Uwekezaji ya Zanzibar**

132. **Mheshimiwa Spika,** Uchumi wowote wa nchi, pamoja na mambo mengine, unategemea kwa kiasi kikubwa uwekezaji ambao utaleta tija kupitia kuzalisha ajira za wananchi wake na hivyo kupatikana kwa kodi ambayo itawezesha utekelezaji wa miradi na shughuli nyengine za nchi. Hata hivyo, changamoto kubwa iliyokuwepo kwa hapa Zanzibar, ni upatikanaji wa mitaji kwa mahitaji ya uwekezaji. Hivyo, Serikali imeamua kuanza matayarisho ya kuanzisha Benki ya Uwekezaji ya Zanzibar ili kukidhi mahitaji ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji wa miradi mbali mbali hapa Zanzibar.

**i. Kufanikisha Mkutano wa Mapitio ya Muda wa Kati wa Utekezaji wa Shughuli za Benki ya Dunia za Kupitia Dirisha la IDA kwa mzunguko wa 19 (IDA-19 Mid Term Review)**

133. **Mheshimiwa Spika,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mara ya kwanza itakuwa mwenyeji wa mikutano mikubwa miwili ya kimataifa katika mwaka 2023. Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Unaohusu Uwekezaji katika Rasilimali Watu (Human Capital Investment Heads of State Summit) utafanyika Mwezi wa Julai, 2023 Jijini Dar-Es-Salaam na Mkutano wa Mapitio ya Mzunguko wa 19 Wa Muda wa Kati utafanyika Zanzibar katika Mwezi wa Disemba, 2023. Kwa upande wa Zanzibar, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watendaji Wakuu wa Benki ya Dunia; wanaendelea na shughuli mbali mbali za matayarisho ya mkutano huu, ambao ni wa kwanza kufanyika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni nafasi ya kipekee kwa Zanzibar, kupata fursa ya kuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa kimataifa kama huu.

134. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano huu, unatarajiwa kuhudhuriwa na washiriki wapatao 350 miongoni mwao wakiwemo Watendaji wa Benki ya Dunia ambao wamekuwa na furaha kubwa sana ya kuiona Zanzibar na kushuhudia yale mazuri yote ambayo wameendelea kuyasikia kuhusu Zanzibar. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango inatarajia kuwa, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kila mmoja kwa nafasi yake, atashirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha Mkutano huu utakaonza tarehe 4 hadi 6 Disemba, 2023 utakamilika kwa mafanikio makubwa sana.

## L. SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### a) Mapato yatakayokusanywa mwaka 2023/2024

135. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Serikali Kwa mwaka fedha 2023/2024 yanakadiriwa kufikia Jumla ya TZS 2,840.85 bilioni, yakiwemo TZS 2,822.85 bilioni kwa Serikali Kuu na TZS 18.00 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Makadirio haya yameongezeka kwa asilimia 9 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2022/2023 ya TZS 2,606.58 bilioni.

#### i. Mapato kwa vyanzo vya Serikali Kuu

136. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekadiria kukusanya TZS 1,419.03 bilioni kutoka katika vyanzo vya ndani ikiwa na ongezeko la asilimia 4 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya TZS 1,369.75 bilioni. Makadirio ya mwaka 2023/2024 yamejumuisha:

a. Makadirio ya TZS 675.60 bilioni zinazotarajiwa kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA);

b. Makadirio ya TZS 520.64 bilioni zinazotarajiwa kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzaniar (TRA);
c. Makadirio ya TZS 201.79 bilioni zinazotokana na Mapato Yasiyokuwa ya Kodi; na
d. Makadirio ya kodi ya mapato kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar ni TZS 21 bilioni.

137. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2023/2024 TZS 717.21 bilioni zitakopwa kwa mkopo maalum utakaochukuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, TZS 686.61 bilioni zinatarajiwa kupokewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwemo mkopo nafuu wa TZS 527.55 bilioni na Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ya TZS 106.62 bilioni, TZS 0.25 bilioni zinatokana na Mfuko wa pamoja wa wafadhili na TZS 52.19 bilioni ni Misaada ya Kibajeti (General Budget Support) .

**ii. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa**

138. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na vyanzo vyake vya ndani (Ada na Tozo) yanayokadiriwa kukusanywa ni TZS 18.00 bilioni.

**b) Mwelekeo wa Matumizi kwa mwaka 2023/2024**

139. **Mheshimiwa Spika;** mgao wa ukomo wa Bajeti ya matumizi katika jumuisho (Aggregate Budget Expenditure) umezingatia kufanikisha shabaha na malengo ya Serikali ambapo mgao huo umefanyika kwa kutumia rejea za nyaraka mbali mbali za kitaifa zikiwemo:
i. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 - 2025;
ii. Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050;
iii. Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) wa mwaka 2021-2026;
iv. Maelekezo na maagizo ya Serikali yanayotolewa na Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Serikali; na
v. Taarifa ya Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2022.

140. **Mheshimiwa Spika,** kulingana na mwelekeo wa Mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali inatarajia kutumia jumla ya TZS 2,840.85 bilioni yakiwemo, Matumizi ya Kazi za Kawaida TZS 1,318.86 bilioni sawa na asilimia 46.42. Matumizi ya Kazi za Maendeleo ya TZS 1,521.99 bilioni sawa na asilimia 53.58 ambapo fedha hizo zimejumuisha TZS 886.00 bilioni ikiwa ni Fedha kutoka Serikalini na TZS 628.80 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zikiwemo (TZS 527.55 bilioni Mkopo, na Misaada ya TZS 101.25 bilioni).

141. **Mheshimiwa Spika, Kiambatanisho Namba.3** kimeonesha uchambuzi wa Sura ya Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

## M. HALI YA UTEGEMEZI KWA MWAKA 2023/2024

142. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikana na Washirika wa Maendeleo itaendelea kutekeleza na kugharamia programu na miradi ya maendeleo iliyopangwa mwaka 2023/2024 na matarajio ni kutumia TZS 628.80 bilioni zitapokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikijuisha Misaada ya TZS 101.25 bilioni. Pamoja na kupokea misaada hiyo, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya ndaniili kupunguza zaidi kiwango cha Utegemezi ambapo kwa mwaka 2023/2024, Kiwango cha Utegemezi kimekadiriwa kufikia asilimia 3.6. Kiwango hicho bado ni himilivu na bado kimo katika mipaka iliyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya C.C.M 2020-2025.

## N. MAZINGATIO YA MAENEO MAHSUSI KWA MATAYARISHO YA BAJETI YA MWAKA 2023/2024

143. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa matumizi. Mifumo hiyo ni pamoja na; Mfumo wa Bajeti na Matumizi (BAMAS), Mfumo wa Manunuzi (eProz), Mfumo wa Ukusanyaji Mapato yasiyokuwa ya Kodi (ZanMalipo) na Mfumo wa ukusanyaji ZIDRAS na ule wa utoaji wa risiti (VFMs). Katika kusimamia upatikanaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo Serikali itaendelea kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji na Tathmini (e-M&E System).

Katika kuhakikisha usimamizi wa mapato, Serikali itaendeleza kuziba mianya ya kodi, kupunguza na kuondosha misamaha ya kodi isiyokuwa na tija.

144. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango itaendelea na jukumu la utafutaji wa rasilimali fedha kugharamia shughuli za Serikali ikiwemo miradi ya maendeleo kupitia mikopo ya ndani na nje, mikopo kutoka taasisi za kifedha, benki za ndani na nje na mifuko ya hifadhi za jamii. Aidha, kutakuwa na mazingatio mahsusi katika bajeti ya mwaka 2023/24 yakiwemo:

i. Ongezeko la Bajeti ya Utekelezaji wa miradi ya maendeleo,
ii. Ongezeko la Pencheni ya Wastaafu na Pencheni Jamii ambapo kuanzia Julai 2023 ulipaji wake utasimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango,
iii. Kuanza kulipa asilimia 3.5 ya mshahara kwa wafanyakazi wa sekta ya umma kwa ajili ya Mfuko Huduma ya Afya.
iv. Kuanza maandalizi ya kuanzishwa kwa Benki ya Uwekezaji ya Zanzibar (ZIB) ambayo pia itatoa huduma za mitaji na uwekezaji kwa wananchi.
v. Kufanya malipo ya amana za wateja wa iliyokuwa FBME kwa upande wa Zanzibar.
vi. Kuendelea na ujenzi wa masoko ya Mwanakwerekwe, Chuini na Jumbi ambayo tayari yanaendelea kujengwa.
vii. Kutoa kipaumbele kwa malipo ya madeni ya Wazabuni, Wakandarasi na Watumishi wa Umma,
viii. Ununuzi wa Vitendea kazi ikiwemo magari na ujenzi wa Ofisi za Serikali; na
ix. Kuzifanyia mageuzi makubwa Taasisi za Umma ili kuongeza ufanisi na kuleta tija.

## O. SHUKRANI

145. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango naomba kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mashirikiano wanayotupatia ambayo yanaimarisha Muungano wetu. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamesaidia Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar katika kuleta maendeleo na wale waliochangia Bajeti yetu ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 zikiwemo Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Jamhuri ya watu wa China, Korea ya Kusini, Kuwait, Malaysia, Misri, Norway, Oman, Qatar, Saudi Arabia, Sweden, Uingereza, Marekani Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu. Pia nayashukuru mashirika na Taasisi zifuatazo: Africa Development Bank (AfDB), Global Fund (GF), BADEA, IFAD, KOICA, UNDP, UNICEF, World Bank (WB), Exim Bank, Global Partnership for Education(GPE), United State Agency for International Development (USAID), United Nation Population fund (UNFPA), Saudi Fund (SF), United Nation For Women (UN Women), Khalifa Fund (KF), Global Fund (GF), MILELE NORAD, UNESCO, Partnership for Child Development International Atomic Energy Agency(IAEA) na United Nation Environment Programme (UNEP).

146. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kuwashukuru viongozi wote wa OR-Fedha na Mipango akiwemo Naibu Waziri wa Fedha **Mhe. Ali Suleiman Ameir.** Pia ninamshukuru Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, **Dkt. Juma Malik Akil** kwa juhudi zake na jinsi anavyoitumikia Serikali yetu ikiwemo maandalizi mazuri ya bajeti hii. Kwa nafasi nyengine naomba nimshukuru Katibu Mtendaji Tume ya Mipango **Dkt Rahma Mahfoudh,** Naibu Katibu Mkuu Fedha na Mipango **Bwana Aboud Hassan Mwinyi** na Mhasibu Mkuu wa Serikali **Dkt. Said Seif Mzee,** Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar **Ndugu Juma Yussuf Mwenda,** Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar Ndugu **Juma Bakari Hassan,** Mkurugenzi wa Sera za Kodi na Fedha **Ndugu Haji Ali Haji,** Kamishna wa Bajeti **Ndugu Saumu Khatib Haji** na Wakurugenzi pamoja na Maafisa wote wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa mashirikiano yao makubwa hadi tunakamilisha Bajeti hii. Katika nafasi hii ya pekee, kwa niaba ya wenzetu wote tunatoa shukrani na pongezi kwa **Ndugu Hurina Mohammed Said,** ambae muda wote amekuwa akisimamia uwasilishwaji wa Bajeti za Wizara mbali mbali muda wote katika kipindi hichi. Tunamshukuru na kumpongeza kwa uzalendo wake

huo aliouonyesha katika miaka yote ambae anakuwa anasimamia Bajeti za Wizara hapa Baraza la Wawakilishi. Amekuwa kiunganishi kizuri baina ya Baraza la Wawakilishi na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango. Mheshimiwa Spika, Nawashukuru sana wasaidizi wetu wote wa Baraza la Wawakilishi ambao wamekuwa wakitusaidia kazi zetu hapa Barazani katika kipindi chote. Nawashukuru na nawapongeza sana kwa jinsi tunavyoshirikiana kutekeleza majukumu ya kuleta Maendeleo ya Taifa letu.

## P. HITIMISHO

147. **Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, naliomba Baraza lako tukufu liridhie Serikali kwa mwaka wa fedha, 2022/2023 kukusanya jumla ya TZS 2,840.85 bilioni( **TZS trilioni mbili bilioni mia nane na arobaini na milioni themanini na tano**). Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani ni TZS 1,419.03 bilioni, Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo TZS 686.61 bilioni, Mikopo ya ndani na nje kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo ni TZS 717.21 bilioni. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu kuridhia kukusanywa TZS 18.00 bilioni kukusanywa na Serikali za Mitaa.

148. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 2,840.85 bilioni( **TZS trilioni mbili bilioni mia nane na arobaini na milioni themanini na tano**) ambapo TZS 1,318.86 bilioni zimeelekezwa kwa ajili ya kazi za kawaida, TZS 1,521.99 bilioni zimeelekezwa kwenye kutekeleza Mpango wa Maendeleo.

149. **Mheshimiwa Spika,** naomba Kutoa Hoja.

**Dkt. Saada Mkuya Salum**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR.**

**Juni,2023.**

## Kiambatanisho Namba.1

**UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA JULAI 2022-MACHI 2023**

**A. MAPATO**

Tarakimu ni "Bilioni"

| MAELEZO | BAJETI 2022/23 | JULAI 2022 -MACHI 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Bajeti | Makadirio | Halisi | % | % miezi |
| ***Mapato ya Ndani*** | ***1,369.75*** | ***1,090.31*** | ***902.57*** | ***66%*** | ***83%*** |
| ZRA | 579.51 | 462.49 | 449.26 | ***78%*** | ***97%*** |
| TRA | 454.06 | 337.03 | 323.01 | ***71%*** | ***96%*** |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 179.48 | 139.35 | 116.30 | ***65%*** | ***83%*** |
| Marejesho kutoka Benki ya Exim | 135.70 | 135.70 | - .0 | ***0%*** | ***0%*** |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 21.00 | 15.75 | 14.00 | ***67%*** | ***89%*** |
| ***Mapato ya Washirika wa Maendeleo*** | **687.95** | **241.52** | **180.49** | ***26%*** | ***75%*** |
| *Mfuko wa Pamoja wa Waafadhili* | 0.23 | 0.23 | 0.23 | ***100%*** | ***100%*** |
| Misaada kutoka Nje | 70.86 | 50.22 | 32.69 | ***46%*** | ***65%*** |
| Mkopo kutoka Nje | 606.86 | 123.64 | 80.14 | ***13%*** | ***65%*** |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 10.00 | 67.43 | 67.43 | ***674%*** | ***100%*** |
| ***Mapato Mengineyo*** | ***515.00*** | ***120.00*** | 0 | ***0%*** | ***0%*** |
| Mkopo wa Ndani | 115.00 | 50.00 | 0 | ***0%*** | ***0%*** |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 400.00 | 70.00 | 0 | ***0%*** | ***0%*** |
| ***Mapato ya Mamlaka za serikali za Mitaa*** | ***33.88*** | ***30.16*** | ***27.59*** | ***81%*** | ***91%*** |
| ***Jumla Kuu*** | ***2,606.58*** | ***1,482.00*** | ***1,110.65*** | ***43%*** | ***75%*** |

**B. MATUMIZI**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ***Matumizi ya Kawaida*** | ***1,220.51*** | ***920.44*** | ***731.17*** | *60%* | *79%* |
| Mshahara Mawizara | 557.95 | 396.50 | 392.14 | *70%* | *99%* |
| Mshahara Ruzuku | 70.73 | 76.55 | 73.30 | *104%* | *96%* |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 265.38 | 211.87 | 94.25 | *36%* | *44%* |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 116.15 | 93.70 | 43.59 | *38%* | *47%* |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 210.30 | 141.82 | 127.90 | *61%* | *90%* |
| ***Matumizi ya Maendeleo*** | ***1,386.07*** | ***418.32*** | ***273.33*** | *20%* | *65%* |
| Fedha za Serikali | 682.54 | 214.30 | 172.27 | *25%* | *80%* |
| Mkopo kutoka Washirika wa Maendeleo | 606.86 | 123.64 | 69.22 | *11%* | *56%* |
| Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 62.79 | 50.22 | 31.84 | *51%* | *63%* |
| ***Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*** | **33.88** | **30.16** | **26.03** | *77%* | *86%* |
| ***Jumla Kuu*** | ***2,606.58*** | ***1,338.76*** | ***1,030.53*** | *40%* | *77%* |

***Chanzo:*** *Afisi ya Rais- Fedha na Mipango*

**Kiambatisho Namba 2**

**MATARAJIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI (LIKELY OUTTURN) KWA MWAKA 2023/2024**

Tarakimu ni TZS "bilioni"

| **A: MAPATO** | | | |
|---|---|---|---|
| **MAELEZO** | **Bajeti Iliyoidhinishwa 2022/23** | **Matarajio 2022/2023** | **% ya Bajeti** |
| **Mapato ya Ndani** | **1,369.75** | ***1,370.35*** | **100%** |
| ZRA | 579.51 | 596.79 | 103% |
| TRA | 454.06 | 426.61 | 94% |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 179.48 | 190.25 | 106% |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 21.00 | 21.00 | 100% |
| Marejesho ya Mkopo (EXIM BANK OF CHINA) | 135.70 | 135.70 | 100% |
| **Mapato ya ODA** | **687.95** | **288.67** | **42%** |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.23 | 0.23 | 100% |
| Ruzuku kutoka Nje | 70.86 | 43.59 | 62% |
| Mkopo kutoka Nje | 606.86 | 106.85 | 18% |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 10.00 | 138.00 | 1380% |
| **Mapato Mengineyo** | **515.00** | ***27.59*** | **5%** |
| Mkopo wa Ndani /TB | 115.00 | | 0% |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 400.00 | 27.59 | 7% |
| ***Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*** | **33.88** | **33.00** | 97% |
| **Jumla Kuu** | **2,606.58** | ***1,719.61*** | **66%** |
| **B:UKOMO WA MATUMIZI** | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | **1,220.51** | **1,003.82** | **82%** |
| Mshahara Mawizara | 557.95 | 560.00 | **100%** |
| Mshahara Ruzuku | 70.73 | 102.80 | 145% |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 265.38 | 136.32 | 51% |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 116.15 | 78.05 | 67% |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 210.30 | 126.65 | 60% |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **1,386.07** | **682.79** | **49%** |
| Fedha za Serikali | 682.54 | 517.93 | 76% |
| Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 669.65 | 164.86 | 25% |
| ***Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*** | **33.88** | **30.80** | 91% |
| **Jumla Kuu** | ***2,606.58*** | ***1,719.61*** | **66%** |

*Chanzo: Afisi ya Rais- Fedha na Mipango*

## Kiambatanisho Namba 3

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | | | | | |
| Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024 | | | | | |
| | | | | Tarakimu ni Bilioni | |
| | **MAPATO SERIKALI KUU** | **2022/2023** | | **2023/2024** | |
| A | **Mapato ya Ndani** | | **1,369.75** | | **1,419.03** |
| | Makusanyo ya Kodi -ZRA | 579.51 | | 675.60 | |
| | Makusanyo ya Kodi - TRA | 454.06 | | 520.64 | |
| | Makusanyo yasiyokuwa ya Kodi | 179.48 | | 201.79 | |
| | Makusanyo ya Kodi za Wanyakazi kutoka SMT (PAYE) | 21.00 | | 21.00 | |
| | Fedha itakayorudishwa na Exim Benki- China | 135.70 | | | |
| B | **Misaada na Mikopo Kutoka kwa washirika wa Maendeleo** | | **687.95** | | **686.61** |
| | Misaada wa Kibajeti | 10.00 | | 52.19 | |
| | Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 70.86 | | 104.94 | |
| | Mikopo nafuu ya Miradi ya Kisekta | 606.86 | | 529.24 | |
| | Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (Basket Fund) | 0.23 | | 0.24 | |
| C | **Mikopo ya Ndani na Nje Kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi wa** | | **515.00** | | **717.21** |
| | Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 400.00 | | 567.21 | |
| | Mikopo ya Hati Fungani | 115.00 | | 150.00 | |
| | **JUMLA YA MAPATO YA SERIKALI KUU (A+B+C)** | | **2,572.70** | | **2,822.85** |
| | | | | | |
| D | **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** | **17.60** | | **18.00** | **18.00** |
| | **Mapato ya Tozo na Ada** | | **33.88** | | |
| | **Mikopo kutoka Taasisi za Fedha** | 16.28 | | | |
| | **JUMLA KUU(A+B+C+D)** | | **2,606.58** | | **2,840.85** |
| | | | | | |
| | **MATUMIZI SERIKALI KUU** | | | | |
| E | **Matumizi ya Kawaida** | | **1,220.51** | | **1,318.86** |
| | Mshahara Mawizara | 557.95 | | 578.71 | |
| | Mshahara Ruzuku | 70.73 | | 97.99 | |
| | Matumizi Mengineyo Mawizara | 265.38 | | 236.94 | |
| | Matumizi Menginiyo Ruzuku | 116.15 | | 85.72 | |
| | Mfuko Mkuu wa Serikali | 210.30 | | 164.00 | |
| | Malipo ya Riba za Ndani na Mitaji | - | | 92.00 | |
| | Michango ya Serikali katika Mifuko ya Jamii | - | | 52.70 | |
| | **Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Makusanyo yao ya Ndani** | | | **10.80** | |
| F | **Matumizi ya Miradi ya Maendeleo** | | **1,352.19** | | **1,521.99** |
| | **Miradi ya Kimkakati** | | | | **915.87** |
| | Fedha za Serikalini | 682.54 | | 495.90 | |
| | Mikopo kwa Washirika wa Maendeleo | 606.86 | | 405.54 | |
| | Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 62.79 | | 14.44 | |
| | **Miradi Mengineyo** | | | | **606.12** |
| | Fedha za Serikali | | | 246.10 | |
| | Mikopo kwa Washirika wa Maendeleo | | | 123.70 | |
| | Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | | | 85.12 | |
| | Fedha iliyotengwa kwa ajili ya ulipaji wa Madeni( Debt amortization fund) | | | 144.00 | |
| | **Fedha inayokusanywa kutoka LGA inayoelekezwa katika Miradi ya** | | | **7.20** | |
| | **JUMLA MATUMIZI YA SERIKALI KUU(E+F)** | | **2,572.70** | | **2,840.85** |
| G | **Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** | **33.88** | | | |
| | **JUMLA KUU YA MATUMIZI (E+F+G)** | | **2,606.58** | | **2,840.85** |
| | *Chanzo: Ofisi ya Rais Fedha na Mipango* | | | | |

## Kiambatanisho Namba 4.

Tarakimu ni TZS "bilioni"

| **A: MAPATO** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MAELEZO** | **Bajeti Iliyoidhinishwa 2022/23** | **Makadirio ya Bajeti 2023/24** | **Makisio 2024/25** | **Makisio 2025/26** |
| **Mapato ya Ndani** | **1,369.75** | ***1,419.03*** | **1,618.83** | **1,866.98** |
| ZRA | 579.51 | *675.60* | 787.09 | 913.90 |
| TRA | 454.06 | 520.64 | 582.66 | 672.67 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 179.48 | 201.78 | 228.08 | 259.41 |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 21.00 | 21.00 | 21.00 | 21.00 |
| Marejesho ya Mkopo (EXIM BANK OF CHINA) | 135.70 | | | |
| **Mapato ya ODA** | **687.95** | **686.61** | **1,046.640** | **435.25** |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.23 | 0.24 | 0.274 | 0.24 |
| Ruzuku kutoka Nje | 70.86 | 104.94 | 67.87 | 143.69 |
| Mkopo kutoka Nje | 606.86 | 529.24 | 890.50 | 203.32 |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 10.00 | 52.19 | 88.00 | 88.00 |
| **Mapato Mengineyo** | **515.00** | **717.21** | **680.00** | **700.00** |
| Mkopo wa Ndani /TB | 115.00 | 150.00 | 180.00 | 200.00 |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 400.00 | 567.21 | 500.00 | 500.00 |
| ***Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*** | **33.88** | **18.00** | **21.00** | **30.00** |
| **Jumla Kuu** | **2,606.58** | ***2,840.85*** | **3,366.47** | **3,032.23** |
| **B:UKOMO WA MATUMIZI** | | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | **1,220.51** | **1,308.06** | **1,415.52** | **1,574.52** |
| Mshahara Mawizara | 557.95 | 631.41 | 638.49 | 692.92 |
| Mshahara Ruzuku | 70.73 | 97.99 | 124.49 | 174.28 |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 265.38 | 236.94 | 213.55 | 256.14 |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 116.15 | 85.72 | 107.77 | 129.32 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 210.30 | 256.00 | 331.22 | 321.86 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **1,352.19** | **1,514.80** | **1,920.02** | **1,423.15** |
| Fedha za Serikali | 682.54 | 742.00 | 961.65 | 1,059.43 |
| Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 669.65 | 628.80 | 958.37 | 363.72 |
| Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo (Debt Services Fund) | | 144.00 | | |
| ***Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*** | **33.88** | 18.00 | 21.00 | 30.00 |
| **Jumla Kuu** | ***2,606.58*** | **2,840.85** | **3,368.54** | **3,030.67** |
| *Chanzo: Afisi ya Rais- Fedha na Mipango* | | | | |